




**Uchunguzi** kifo cha anayedaiwa kujinyonga polisi wakwama kuanza

UKURASA 3




UKURASA 11


# Nipashe

Jumamosi Februari 18, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0581225

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




# Wagonjwa wapewa dawa zilizokwisha muda wa matumizi

UKURASA 2

UKURASA WA 4

## JK MWENYEKITI MPYA WA TUZO YA CHAKULA AFRIKA



RAIS wa Awamu ya Nne wa Tanzania, Dk. Jakaya Kikwete, ametangazwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Tuzo ya Chakula Afrika (AFP)...

## Sheria sasa kufumuliwa kuwabana wanaotupa watoto wachanga

UKURASA 10




Rais Samia Suluhu Hassan, akifuatilia kwa makini wakati Mwenyekiti wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye (kulia), akizungumza katika Mkutano Maalum wa Wakuu wa EAC, uliofanyika katika Jengo la Usalama na Amani la Julius Nyerere, Makao Makuu ya Umoja wa Afrika (AU), jijini Addis Ababa, Ethiopia jana. **PICHA: IKULU**

## Mchengerwa aanza na mambo matatu nyeti Maliasili, Utalii

UK.2

**MICHEZO** **TUTAWASHA MOTO LEO** UK.24

**MAONI** UK.6



Mwenyekiti wa kikundi cha vijana wajasiriamali cha kutengeneza magodoro, Ally John, akionyesha kiwanda chao kilivyoteketea kwa moto na kupoteza vitu vyote vyenye thamani ya Sh. milioni 93, katika mtaa wa Viwandani, Manispaa ya Shinyanga, mapema wiki hii. Kwa mujibu wa John, kiwanda hicho kilikuwa kikiendeshwa kwa mkopo wa asilimia 10 kwa vijana wa Sh. milioni 40 uliotolewa na halmashauri. **PICHA: MARCO MADUHU.**

# Wagonjwa wapewa dawa zilizoisha muda matumizi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Shinyanga imebaini Bohari ya Dawa (MSD) imeshindwa kupeleka dawa kwenye vituo vya afya licha ya kulipwa fedha.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani Shinyanga, Donasian Kessy alibainisha hayo jana wakati akitoa taarifa kwa waandishi wa habari kwa kipindi cha robo ya pili ya mwaka wa fedha 2022/23 kuanzia Oktoba hadi Desemba.

Alisema kuwa katika kipindi hicho, pia walifanya ufuatiliaji wa uchambuzi wa mfumo kuhusu ununuzi na ugavi wa dawa kwenye hospitali ya wilaya, vituo vya afya na zahanati za Manispaa ya Kahama na kubaini kuwapo mianya ya wizi wa dawa.

Alisema kuwa katika uchunguzi huo walibaini kuwa MSD ilikata fedha na kuonyesha ilituma dawa, lakini baada ya kufuatilia hawakuona dawa zozote zilizotumwa.

"Vitu ambavyo tumevibaini kwenye uchambuzi huu wa mfumo wa ununuzi na ugavi wa dawa ni kuwa MSD wamekuwa wakikata fedha kwa baadhi ya vituo bila mzigo husika kufika kituoni na wala invoice (ankara ya malipo) kusainiwa vituoni na kupelekwa mzigo hewa," alisema Kessy.

"Kitu kingine ambacho tumekibaini watumishi wa idara ya afya hawajazi kumbukumbu za ununuzi na ugavi wa dawa na vifaa tiba, kuwapo uingizwaji wa dawa zilizomaliza muda kwenye huduma za afya, vituo vya afya na zahanati kuazimana dawa na kusababisha wizi kwa sababu haziingizwi katika kumbukumbu," alibainisha.

Kiongozi huyo alisema hatua ambazo wamependekeza zichukuliwe ni pamoja na kuwapo ukaguzi wa mara kwa mara wa dawa kwenye huduma za afya, watumishi wa kada ya afya wapatiwe elimu ya umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu za uingizaji na utoaji wa dawa.

Kessy alisema TAKUKURU pia imefanya uchambuzi wa mfumo kuhusu uendeshaji wa masoko ya biashara kwenye Manispaa ya Kahama na kubaini kuwapo upotevu wa fedha nyingi za serikali.

Alisema walibaini wafanyabiashara 234 kwenye Soko la CDT hawalipi kodi wala ushuru, huku baadhi ya watumishi wakihodhi vibanda na meza kwa majina mengine.

Alitoa wito kwa wananchi mkoani Shinyanga kuendelea kutoa taarifa za rushwa kwa kupiga simu bure 0738150196 au wafike kwenye ofisi za taasisi hiyo ili hatua zichukuliwe mapema na kuzuia rushwa na kupata haki zao bila ya kutoa fedha yoyote.

**JICHO LA CAG**

Wakati hayo yakiendelea mkoani Shinyanga, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) aliripoti Machi mwaka jana kuwapo dawa zenye thamani ya Sh. bilioni 23.04 zilizokwisha muda wake kwenye maghala ya MSD na Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

CAG Charles Kichere anafafanua kuwa kiwango cha kwisha muda wa dawa kwa mwaka wa fedha 2020/21 kilikuwa asilimia tano ya gharama za mauzo ya Sh. bilioni 196.83 sawa na kiwango kilichoripotiwa mwaka 2019/20 (cha asilimia tano).

"Kiwango hiki kimezidi kiwango kinachotakiwa kwa asilimia mbili kama kilivyoelezwa katika Aya ya 7.3.3 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za MSD wa mwezi Juni 2018.

"Uchambuzi wangu pia ulibaini kuwa MSD ilikuwa na jumla ya bidhaa 7,676,436 za thamani ya Sh. bilioni 22.8 zilizopitwa na muda ambazo zilikuwa kwenye maghala ya MSD kuanzia tarehe 16 Aprili 2000 hadi 30 Juni 2021.

"Aidha, nilibaini MSD ilipokea fedha kutoka kwa wafadhili ambazo ni dola za Marekani 239,023.92 ili kugharamia kuharibu dawa za kupunguza makali ya VVU/UKIMWI.

"Ingawa ruhusa ya kuteketeza dawa hizo ilishatolewa na Wizara ya Fedha na Mipango tangu tarehe 7 Oktoba 2021, dawa hizo hazikuharibiwa hadi wakati wa ukaguzi mwezi Desemba 2021.

"Pia, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili nilibaini kuwapo kwa ucheleweshaji wa kuomba vibali vya uhakiki wa vifaa tiba vya kuanzia mwaka 2014 hadi Juni 2020, ambavyo ni dawa, vifaa vya matumizi ya upasuaji na vitendanishi vilivopitwa na muda kutoka katika mamlaka za serikali zinazohusika.

"Vifaa tiba hivi vilivyopitwa na wakati/visivyotumika vilikuwa vya thamani ya Sh. milioni 235. Maombi ya vibali yalitumwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali tarehe 29 Septemba 2020 na 22 Septemba 2020," anabainisha.

CAG anaendelea kufafanua kuwa hali hiyo ni kinyume cha Aya ya 26 ya Mwongozo wa Usimamizi wa Mali za Umma (Toleo Lililorekebishwa la Mwaka 2019) inayotaka maombi kuwasilishwa kwa Mlipaji Mkuu wa Serikali ndani ya siku 21 za kazi baada ya hasara kutokea.

Anasema MSD na MNH zinaingia kwenye gharama zisizo za lazima za uhifadhi na ulinzi wa bidhaa kwenye maghala ambazo hazitumiki, pia kuendelea kuwapo kwa bidhaa zilizoisha muda wake kunahatarisha afya za watumishi wanaofanya kazi kwenye maghala hayo.

"Ninapendekeza MSD iteketeze dawa zilizoisha muda ambazo kibali chake kimetolewa na ishirikiane na MNH kufuatilia vibali vya kuteketeza dawa na vifaa tiba ambavyo vimepitwa na muda," CAG anawasilisha hoja yake.

# Mchengerwa aanza na mambo matatu Utalii

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Mohamed Mchengerwa, ameanza kazi rasmi kwa kuwataka watumishi wa wizara hiyo kujipanga katika kuhifadhi rasilimali za nchi, kuongeza kasi ya kutangaza vivutio vya utalii na kufanya kazi kwa bidii.

Mchengerwa alisema hayo jana wakati wa hafla ya uzinduzi wa magari 22 yatakayotumika katika shughuli za uhifadhi, iliyofanyika kwenye ofisi za makao makuu ya Mamlaka ya Uhifadhi na Usimamizi Wanyamapori Tanzania (TAWA), mkoani Morogoro.

Waziri Mchengerwa aliwataka watumishi hao kujipanga kwenda kuhifadhi vyema maliasili za nchi pamoja na kukabiliana na changamoto wanazokutana nazo kwa kuzitatua inavyostahili.

"Tujipange kwenda kuhifadhi sana, tuhifadhi kwelikweli. Zile changamoto tunazoweza kuzitatua ni lazima tuzitatue. Nataka kila mmoja wetu akafanye kazi kwenye eneo lake na kama utatakiwa kuwapo kwenye eneo lako saa 6:00 mchana, basi uwapo," alisisitiza.

Aidha, Mchengerwa alisema mbali na shughuli za kudhibiti ujangili, magari hayo yatumike pia katika kujenga uhusiano mzuri na wananchi wanaozunguka maeneo ya hifadhi.

Pamoja na kazi nzuri za uhifadhi zinazofanywa na TAWA na taasisi zingine za uhifadhi, Mchengerwa alisema bado asilimia 21 ya pato la Taifa linalochangiwa na Wizara ya Maliasili na Utalii ni dogo kulinganishwa na wingi wa rasilimali zilizoko katika Taifa.

Kutokana na hali hiyo, aliwahimiza viongozi na watumishi kupitia taasisi zao, kuongeza kasi ya kutangaza vivutio vya utalii ili kuongeza pato la taifa.

Mchengerwa aliushukuru uongozi wa TAWA kwa kutenga fedha ambazo zimewezesha kununua magari hayo ambayo yatatumika katika shughuli za doria, kudhibiti ujangili na wanyamapori wakali na waharibifu.

Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Hassan Abbas, aliwataka watumishi kujipanga na dhana nzima ya uhifadhi wa misitu, wanyamapori na vivutio vya utalii huku wakiendeleza ushawishi wa kupata watalii kwa sababu wizara hiyo ndio inayoiletea serikali fedha za kigeni.

"Tuheshimu sana watalii wanapokuja nchini kwa sababu wanatumia fedha na muda wao kuja kwetu kujifunza vitu lakini lazima tufanye ushawishi na kutangaza vivutio ili tukusanye mapato mengi ya utalii ya kumsaidia Rais wetu Samia Suluhu Hassan kuleta maji au umeme," alisema Dk. Abbas.

Viongozi wengine waliohudhuria hafla hiyo ni Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara, Juma Mkomi, na Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu, Prisca Lwangili.

# Uchunguzi mwili aliyedaiwa kufia polisi wakwama kuanza

**Na Grace Gurisha**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kivukoni, Kinondoni Dar es Salaam, Machi 3, mwaka huu, inatarajia kuanza uchunguzi wa chanzo cha kifo cha Stella Moses, aliyefia katika Kituo cha Polisi Mburahati kwa madai kuwa alijinyonga.

Uchunguzi huo ulishindwa kuanza jana mbele ya Hakimu Mkazi Mfawidhi, Franco Kiswaga wa mahakama hiyo, kwa sababu wakili wa wajibu maombi ambaye ndiye anayeendesha shauri hilo ana udhuru, hivyo hakuwapo mahakamani.

Wakili wa waleta maombi, Peter Madeleka, alidai kuwa shauri hilo liliitwa kwa ajili ya kuanza kwa uchunguzi wa mwili wa Stella kutokana na uamuzi wa mahakama uliotolewa Desemba 19,2022 na pia wako tayari kuendelea.

Baada ya Madeleka kudai hivyo, Wakili wa wajibu maombi, Deborah Mushi, alidai kuwa juzi ndiyo walipokea hati ya wito wa mahakama, hivyo wanaomba wapewe nyaraka na pia wanaomba wiki mbili ili wajiandae kama watawasilisha chochote.

Akijibu hoja hiyo, Madeleka alidai kuwa hatua shauri lilipofikia na uamuzi wa mahakama uliotolewa mwaka jana, hakuna nyaraka yoyote inayohitajika, hivyo jana ilikuwa kwa ajili ya uchunguzi.

"Tunaomba mahakama itupe maelekezo kwamba uchunguzi unafanyikaje kwa sababu sina jalada na wakili anayesimamia shauri hili, ana udhuru kwa hiyo tunaomba tupangiwe tarehe nyingine, " alidai Mushi.

Hata hivyo, Wakili Madeleka alipinga kuahirishwa kwa shauri hilo kwa madai kuwa hakuna sababu za msingi zilizotolewa kwa kuwa kuna utaratibu wa kuahirisha shauri kama hilo.

"Nimekuja leo kama wakili wa serikali kwa kumwakilisha mwenzangu ambaye ana udhuru, ndiyo maana nimeomba ahirisho na hapa jaji ananisubiri Mahakama Kuu kwenye kesi ya mauji," alidai Mushi.

Hakimu Kiswaga alisema amesikiliza hoja za pande zote mbili na kwa busara ya mahakama inamwongoza awasikilize wiki ijayo, Jumatatu au Jumanne.

Shauri hilo liliahirishwa hadi Machi 9 na hakimu alitoa ahirisho la mwisho kuwa siku hiyo lazima uchunguzi ufanyike.

Machi 22, 2022 shemeji wa marehemu, Emmanuel Kagongo, alifungua shauri dhidi ya Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP), Kamanda wa Polisi Kanda Maalum Dar es Salaam (ZPC), Kamanda wa Polis Mkoa wa Kipolisi Kinondoni (RPC), Mkuu wa Polisi Wilaya ya Kipolisi Mburahati (OCD).

Wajibu maombi wengine ni Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), akiomba ufanyike uchunguzi huru ili kujua ukweli wa mazingira ya kifo cha shemeji yake.

Katika uamuzi wake, Kiswaga alisema alipitia kiapo cha Mwanasheria Mkuu wa Serikali (AG), Hospitali ya Taifa Muhimbili na RPC Kinondoni na kubaini kuwa kulikuwa hakuna ubishi kama Stella Desemba 20,2020 alifia katika Kituo cha Polisi Mburahati.

Pia alisema kibali cha mazishi kinaonyesha tarehe hiyo na ni eneo gani ambalo Stella alifia na kwa mantiki hiyo mahakama inalo jukumu la kutoa amri ya kufanyika uchunguzi wa mwili.

Kwa mujibu wa hati ya kiapo chake, Kagongo anadai kuwa Desemba 28, 2020 Idara ya Vizazi na Vifo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili ilitoa kibali cha mazishi kwa Eliud Ernest Kagongo chenye namba 1097179 kuridhia mazishi ya mwili wa Stella Moses.

Ilidaiwa kuwa Stella alikwenda katika kituo hicho cha polisi alikojisalimisha baada ya kupata taarifa kuwa alikuwa anahitajika. Polisi walidai kuwa alijinyonga lakini ndugu wa marehemu walipinga taarifa hiyo wakidai kuwa kuna utata wa kifo hicho.

# Serikali yaonya madaktari kutegemea ubunifu wa nje

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imewataka madaktari bingwa wa Tanzania kuwa wabunifu na kugundua mbinu mpya za matibabu ili kuwavutia mataifa mengine kuja kujifunza nchini badala ya kuwa tegemezi wa ubunifu wa wengine.

Vilevile, imesema kuna umuhimu kuwekeza kwa watu wenye akili kubwa ili wagundue teknolojia mpya mbalimbali zikiwamo za tiba badala ya kutegemea za nje kila wakati.

Jijini Dar es Salaam jana, Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel alitoa kauli wakati akifungua mkutano wa kimataifa unaohusu shambulio la moyo ulioandaliwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI).

Alisema kuna umuhimu wa kuwekeza kwenye rasilimali watu kwa kuwa uzoefu unaonyesha kuwa nchi nyingi zimeendelea si kwa sababu ya kuwa na rasilimali nyingi, bali kwa kuwa na watu wenye akili nyingi.

"Kuna umuhimu wa kuwatambua watu wetu wenye akili kubwa na kuwekeza kwao, wenzetu walifanya hivi tangu zamani na watu hao wamewasaidia kugundua vitu vingi ambavyo wengine wameshindwa.

"Ili tuendelee haraka, lazima tugundue vitu vipya. Kwa mfano, ifikie wakati tuseme mbinu hii mpya ya tiba imegunduliwa na Dk. Peter Kisenge wa JKCI na mbinu hii mpya ya tiba imegunduliwa na Prof. Mohamed Janabi au tuseme dawa hii imegunduliwa Tanzania na chanjo hii imetengenezwa na Mtanzania," alisema Dk. Mollel.

Alisisitiza kuwa lazima kuwekwe mkakati wa kitaifa wa kuwatambua wagunduzi wa ndani ili baadaye Tanzania isaidie mataifa mbalimbali kuhusu teknolojia mpya badala ya kila siku kutegemea za wengine.

Dk. Mollel pia aliwataka Watanzania kujenga utamaduni wa kupima afya ya moyo mara kwa mara badala ya kusubiri mpaka hali inapokuwa mbaya, akionya kuwa uzoefu unaonyesha kuwa wengi hufariki dunia.

Vilevile, Dk. Mollel alisema asilimia saba ya vifo vyote vinavyotokea nchini, vinasababishwa na shambulio la moyo, hivyo kuwataka wananchi kujenga utamaduni wa kupima afya mara kwa mara.

Alisema kwa Tanzania ikiwa asilimia saba, kidunia asilimia 30 ya vifo vyote vinatokana na magonjwa ya shambulio la moyo, hivyo kuna umuhimu madaktari kutoa elimu kwa umma kuhusu hatua za kuchukua wanapoona dalili za ugonjwa huo.

Alisema JKCI ni taasisi kubwa kwenye Ukanda wa Afrika Mashariki na Kati kutokana na kufanya upasuaji wa kitaalamu wa moyo ambao miaka michache iliyopita wagonjwa walilazimika kwenda India na mataifa mengine kupata huduma hiyo.

Alisema kuna umuhimu wa wananchi kupata elimu kuhusu namna ya kubaini ugonjwa huo mapema na kwenda kupata huduma ya matibabu ili wasipoteze maisha kwa wingi.

"Madaktari hawa wanazungumzia mbinu mbalimbali za kibingwa ambazo zitatumika kutibu kwa urahisi na kwa usalama zaidi na kikubwa, serikali yetu imewekeza fedha nyingi sana kwenye taasisi hii, ndiyo maana unaona wenzetu wanakuja kujifunza hapa.


IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI

LAND CASE NO.4 OF 2021

J.S.KHAMBHAITA.......................................... ..............................PLAINTIFF

VERSUS

SHEILA CHRISTOPHER DANIEL & OTHERS................................DEFENDANT

TO: HAMIS ABDALLAH JUMA .

NOTICE FOR MENTION.

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 10th March ,2023 at 09:00 a.m. before Honourable **Judge in charge.**

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Mwananchi newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this **14th day of February ,2023**

GIVEN UNDER 2023

DEPUTY REGISTRAR

217286302



IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
MOSHI DISTRICT REGISTRY
AT MOSHI

LAND CASE NO.4 OF 2021

J.S.KHAMBHAITA.......................................... ..............................PLAINTIFF

VERSUS

SHEILA CHRISTOPHER DANIEL & OTHERS................................DEFENDANT

TO: ELINE WILFRED ABRAHAM NYANGE .

NOTICE FOR MENTION.

**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 10th March ,2023 at 09:00 a.m. before Honourable Judge in charge.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe newspaper.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

GIVEN UNDER my hand and seal of the Court this 14th day of February ,2023

GIVEN UNDER 2023

DEPUTY REGISTRAR

217286302



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
18.02.2023

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya **Alhamisi tarehe 23-02-2023** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mzigo wenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port** kuelekea **Ruvuma kupitia Mingoyo,** gari hiyo ina namba za usajili: **T 835 DSC / T 139 CHN**

2. Gari hiyo ina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu** - **mita 18.00**
   **Upana** - **mita 5.55**
   **Kimo** - **mita 4.80**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, hadi Ruvuma kupitia Mingoyo, Nangurukuru,Lindi,Masasi, Songea mpaka Ruvuma** gari itasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

# Mradi wakwama licha ya serikali kutoa Bil. 3/-

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MRADI wa ujenzi wa Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Mkoa wa Singida inayojengwa Kata ya Solya wilayani Manyoni mkoani Singida ambayo serikali ilishatoa Sh. bilioni tatu kwa ajili ya awamu ya kwanza ujenzi wake, haujakamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya mfumo wa malipo.

Kukwama kwa ujenzi huo kumebainika baada ya Katibu Tawala wa Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko kutembelea kukagua mradi huo akiwa ameambatana na Sekretarieti ya Mkoa na kukuta mafundi wengi hawaendelei na kazi ya ujenzi.

Kaimu Ofisa Elimu Wilaya ya Manyoni, Andrew Coromany alisema ujenzi wa shule hiyo umekwama kukamilika kwa wakati kutokana na changamoto ya mfumo wa malipo ambayo imekuwapo tangu mwishoni mwa mwaka jana.

Alipoulizwa kama kutolipwa kwa mafundi hao kutokana na ukosefu wa fedha, Ofisa Elimu alibainisha kuwa kati ya Sh. bilioni tatu zilizoletwa na serikali kwa awamu ya kwanza, zilizobaki ni Sh. bilioni 1.49 na kwamba tatizo ni ofisi ya mhasibu kuchelewesha malipo kwa mafundi.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Mwaluko, alisema anashangaa kukwama kuendelea kwa ujenzi wa shule hiyo wakati fedha zipo na kwamba waliahidi katika kikao chao na Kamati ya Bunge kwamba ujenzi utakamilika Desemba 2022 ili wanafunzi waanze masomo Januari mwaka huu.

Mwaluko alisema kutokana na kukwama kwa ujenzi wa shule hiyo, itabidi yeye na timu yake warejee tena wilayani Manyoni kuzungumza na viongozi wote wa wilaya hiyo kabla ya Februari 27 mwaka huu.

Mwekahazina wa Halmashauri ya Manyoni, Hadhil Nyayunda, alipoulizwa na Nipashe sababu za kuchelewesha malipo, alisema hakuna malipo yoyote ya mafundi yaliyopelekwa kwenye ofisi yake na kukwamishwa.

"Mchakato wa malipo kwa mafundi unaanzia kwenye Kamati ya Ujenzi, unakwenda kwa Mhandisi wa Wilaya na mimi DT nikishaletewa, sina sababu yoyote ya kukwamisha malipo wakati fedha zipo na mradi huu ni muhimu sana," alisema. Wakati Katibu Tawala na viongozi wakikagua mradi huo, walibaini baadhi ya majengo ambayo ujenzi wake ulishaanza yakiwa yamepinda, mfano jengo la bweni, hali ambayo ilitia shaka uimara wa jengo hilo.

Agost mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa aliweka jiwe la msingi la mradi wa shule hiyo ya wasichana ambayo hadi kukamilika kwake, inatarajiwa kugharimu Sh. bilioni nne.

# JK Mwenyekiti mpya wa Tuzo ya Chakula Afrika

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Awamu ya Nne wa Tanzania, Dk. Jakaya Kikwete, ametangazwa kuwa Mwenyekiti mpya wa Tuzo ya Chakula Afrika (AFP).

Taarifa iliyopatikana jana kutoka Addis Ababa, Ethiopia ambako unafanyika Mkutano wa Wakuu wa Nchi wa Umoja wa Afrika (AU) ilisema Kikwete anachukua nafasi ya Rais wa zamani wa Nigeria, Jenerali Olusegun Obasanjo, ambaye amekuwa kwenye nafasi hiyo tangu mwaka 2016.

Akimkaribisha mrithi wake, kwa mujibu wa taarifa hiyo, Obasanjo alielezea matumaini yake kuwa kutokana na kazi yake, Kikwete ameonyesha uwezo na kujitoa kwa dhati katika kuleta mabadiliko ya kilimo barani Afrika.

"Nampongeza Dk. Kikwete kwa kuteuliwa kuwa Mwenyekiti wa Tuzo ya Chakula Afrika. Kupitia uongozi wake, nina imani kwamba Afrika itaendelea kuibua na kuendeleza mikakati ya masuala ya mifumo ya chakula na kuwaondoa watu kutoka kwenye umaskini kupitia ukuaji jumuishi na maendeleo endelevu," alisema Obasanjo.

Kikwete ana rekodi nzuri kama mchangiaji mkubwa katika mageuzi ya mfumo wa chakula Afrika. Alipokuwa Rais wa Tanzania Kikwete aliongoza mpango wa mageuzi ya kilimo Tanzania uliojulikana kama 'Kilimo Kwanza', ambao ulilenga kukuza tija na manufaa kwa wakulima wadogo.

Wakati wa ungozi wake pia alianzisha Jukwaa la Maendeleo ya Kilimo kwa Ukanda wa Kusini mwa Afrika (SAGCOT), unaojumuisha sekta ya umma na binafsi katika kuvutia na kuendeleza uwekezaji wa sekta binafsi katika sekta ya kilimo Tanzania.

Baada ya kustaafu, Kikwete kupitia taasisi yake ya Jakaya Mrisho Kikwete Foundation, amekuwa akishirikiana na wakulima na watafiti kuendeleza mipango na mikakati ya kuongeza mazao na tija kwa wakulima wadogo na wale wanaojihusisha na biashara kilimo.

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

**MAOMBI YA KUWASILISHA NIA KWA AJILI YA KUSANIFU NA KUTEKELEZA PROGRAMU YA KUFANYA UTAFITI NA KUREJESHA MSITU WA MIKOKO NA ONGEZEKO YAKINIFU LA BIOANUAI YAKE KATIKA BAHARI YA MKOA WA TANGA KATIKA MRADI WA BOMBA LA MAFUTA GHAFI LA AFRIKA MASHARIKI (EACOP) KUMB NA – REQ-00000157**

Kampuni ya EACOP inazialika kampuni zenye uzoefu na sifa kuwasilisha maombi ya nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza **''Kusanifu na Kutekeleza Programu ya Kufanya Utafiti na Kurejesha Msitu wa Mikoko na ongezeko yakinifu la bioanuai yake katika Bahari ya Mkoa wa Tanga"** katika Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP). Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litalofukiwa ardhini, linalokatisha mipaka ya nchi mbili ili kusafirisha mafuta ghafi kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda hadi Pwani ya Mashariki mwa Tanzania kwa ajili ya Kwenda katika Masoko ya Kimataifa. Bomba litaanzia eneo la Kabaale Wilaya ya Hoima, nchini Uganda, hadi eneo la Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania.

**MAELEZO MAFUPI YA MAWANDA YA HUDUMA**

Kituo cha baharini cha Mradi wa EACOP cha Rasi ya Chongoleani kitakuwa na Sehemu iliyo nchikavu ya kuhifadhia mafuta, bandari (njia ya juu ya maji) yenye urefu wa kilomita 2 kuelekea ndani ya bahari, na sehemu ya kupakilia mafuta mwisho wa bandari (njia) hiyo. Katika ujenzi wa njia (bandari) hiyo na matumizi yake sehemu ndogo ya habitati ya Msitu wa Mikoko itaweza kuathiriwa. Mpango wa Utekelezaji wa Bioanuwai (Biodiversity Action Plan) umeshaandaliwa na umeonesha kiwango cha awali cha maeneo yatakayoweza kuathirika. Vifo vya mikoko magondi au mikoko myekundu (Rhizophora mucronate) vimetokea na kuandikwa mwaka 2021 na havihusiani kabisa na shughuli za EACOP.

Inahitajika Kampuni/Taasisi ya kufanya usanifu na utekelezaji wa programu ya urejeshaji wa habitati ya msitu wa mikoko; na kutafiti juu ya sababu zilizopelekea kufa kwa mikoko myekundu katika mdomo wa Mto Zigi, na matokeo ya utafiti huo yatumike katika utekelezaji wa urejeshaji wa mikoko katika Ghuba ya Tanga na kaskazini mwa Tanzania kwa ujumla ikilenga ongezeko halisi (Net Gains) na ikizingatia vigezo na mbinu bora. Njia ya kuyafikia hayo inatakiwa iwe shirikishi ambapo hatua zote zitajumuisha wadau wa ndani na vikundi vyengine, ikiwa ni pamoja na jumuiya za mitaa, taasisi za serikali na mashirika ya kiraia. Maamuzi ya kutekeleza njia au mbinu zitakazokubaliwa yanapaswa kuzingatia takwimu za kisayansi na kuhakikisha ubora wa maamuzi hayo kulingana na hali ya kijamii na mazingira yaliyopo hivi sasa na mwelekeo wa baadae.

**VIGEZO MUHIMU**

Kampuni zinazowasilisha nia zinapaswa kutuma maombi pamoja na nyaraka zifuatazo:

- Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na shughuli za ushirikishaji jamii (kwa mfano urejeshaji wa habitati za baharini unaoshirikisha jamii).
- Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kupanga, kusanifu na kutekeleza programu za uendelezaji wa urejeshaji wa misitu ya mikoko, utafiti wa kufa kwa mikoko, kuanzisha vitalu vya miche ya mikoko, kufanya kazi kwa kushirikiana na kujenga uwezo wa jamii za pwani, kufanya utafiti, ufuatiliaji na utengenezaji wa ramani za mtandao wa misitu ya mikoko.
- Mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanana na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopitaLeseni ya biashara.
- Wasifu wa watendaji watakaohusika katika Mradi ikiwa ni Pamoja na nakala za vyeti vyao, kiwango cha elimu, uzoefu na uwezo wa kutoa huduma inayohitajika.
- Leseni inayofaa kutoka kwa mamlaka husika ya ndani ya nchi kwa ajili ya utoaji wa huduma hii
- Uthibitisho wa Usajili toka Mamlaka ya Mapato ya Tanzania (TRA) na Cheti cha Uthibitisho wa Malipo ya Kodi cha mwaka wa hivi karibuni.
- Usajili katika Kanzi Data ya Watoa Huduma wa Ndani ya EWURA (LSSP) au ushahidi thabiti wa maombi ya usajili wakati wa uwasilishaji wa maombi ya nia hii iliyotangazwa.
- Kufuata/kukubaliana na kanuni za Wazawa za Mambo ya Petroli za Tanzania.
- Uwezo wa kifedha wa kutoa huduma zinazohitajika ikiwa ni Pamoja na kuwakilisha hesabu za fedha za miaka mitatu iliyopita.
- Uthibitisho kutoka mfumo wa usimamizi wa QHSE, taasisi na mchakato kulingana na viwango vya ndani na vya ki-sekta vinayotumika kwa kazi hii.
- Uthibitisho wa kukubaliana na sera za Haki za Binadamu, na kupinga rushwa na ufisadi.

Kampuni zenye nia uwezo na rasilimali ya kutoa huduma zilizotajwa hapo juu zinatakiwa kutuma maombi ya nia yaliyoandaliwa kwa lugha ya Kiingereza pamoja na nyaraka zilizobainishwa hapo juu kupitia barua pepe: **procurement.tz@eacop.com (ukubwa usiozidi MB20) kabla au si zaidi ya saa 11:00 jioni Majira ya Afrika Mashariki, tarehe 2nd March 2023.** Kichwa cha cha barua pepe kiwe: [REQ-00000157] _ 'Kusanifu na Kutekeleza Programu ya Kufanya Utafiti na Kurejesha Msitu wa Mikoko na ongezeko yakinifu la bioanuai yake katika Bahari ya Mkoa wa Tanga katika Mradi wa EACOP.

Maombi yote ya kuonesha nia yawe kati ya kurasa 10 hadi 20.

Maombi yote lazima yawasilishwe kwa lugha ya Kiingereza.

**Muhimu:** EACOP itapitia na kuchambua nyaraka ziizotumwa na makampuni yalioonesha nia kulingana na EOI hii, na kisha kufanya tathmini kulighana na vigezo vya ndani vya EACOP ili kubaini makampuni yenye sifa yatakayojumuishwa kwenye orodha ya awali ya makampuni yenye vigezo. Mwaliko kwa Makampuni kutuma maombi ya zabuni utatumwa kwa Makampuni ya awali yenye vigezo baada ya makampuni hayo kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA). Kampuni ya EACOP LTD ina haki ya kuteua au kukataa kampuni na kubaki na maamuzi yake bila kutoa sababu kwa kampuni husika.

# Kongamano Tanzania, EU kuibua fursa uchumi

**Na Romana Mallya**

KONGAMANO la Kwanza la Biashara kati ya Tanzania na Umoja wa Ulaya (EU) linalotarajiwa kufanyika Dar es Salaam, litaongeza fursa ya kuvutia wawekezaji, teknolojia, utaalamu na nchi kuongeza biashara katika soko la EU, imeelezwa.

Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, Dk. Ashatu Kijaji, aliyasema hayo jana Dar es Salaam wakati akizungumzia kongamano hilo linalotarajiwa kufanyika kwa siku mbili kuanzia Februari 23, mwaka huu.

"Ninatarajia kuona kongamano hili la biashara la kwanza kuwa fursa ya kuvutia wawekezaji, teknolojia na utaalamu katika nchi yetu na kuvutia biashara na uwekezaji kutoka duniani kote katika sekta za nishati, madini na kilimo endelevu," alisema.

Dk. Kijaji alisema kongamano hilo ambalo limeandaliwa na wizara kwa kushirikiana na EU pamoja na sekta binafsi, linatarajiwa kuhudhuriwa na zaidi ya washiriki 600 kutoka nchi za EU na Watanzania.

"Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango anatarajia kulifungua akimwakilisha Rais Samia Suluhu Hassan. Kongamano hili litahudhuriwa na mawaziri wanane kutoka Tanzania Bara na Zanzibar. Pia kutashuhudiwa utiaji saini wa hati za makubaliano mbalimbali ya uwekezaji baina ya Tanzania na EU," alisema.

Waziri alisema lengo lake ni kuwaunganisha washiriki hao ili kuwawezesha kubadilishana uzoefu, kushirikiana na watoa maamuzi na kukutana na wawekezaji wanaofaa pamoja na kujenga uelewa kuhusu fursa za uwekezaji zilizopo sekta ya umma na binafsi.

Kwa mujibu wa Kijaji, kongamano hilo litafungwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, ambaye atashuhudia utiaji saini wa mikataba ya fedha na hati za makubaliano.

Alisema mbali na mawaziri, pia litahudhuriwa na mabalozi sita wa Tanzania katika nchi za Umoja wa Ulaya ambao watashiriki katika vikao vya majadiliano kati ya serikali na biashara.

Waziri huyo alisema wanatarajia hati za makubaliano zitakazotiwa saini zitaendeleza na kukuza biashara kati ya nchi hizo, kuongeza ajira kwa vijana na kuchangia katika ukuaji wa uchumi wa nchi.

"Wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Tanzania mtumie fursa hii vizuri kuendeleza na kukuza biashara yenu kwa kujifunza mbinu mpya za kibiashara, kupata wabia na masoko ya bidhaa zetu nje ya nchi," alisema.

Alisema katika soko la EU wamepeleka zaidi bidhaa za kilimo, mifuko na madini yakiwa kwenye malighafi ingawa si kwa kiwango kikubwa.

"Kutoka kwao mnafahamu ndege tunanunua EU, dawa ambazo zinatusababishia kulipa fedha nyingi kuliko kile ambacho tunapata, ni wito wetu kwa wawekezaji wa Tanzania kuendelea kutumia fursa hizi ili tuongeze thamani ya bidhaa zetu," alisema.

HABARI KITAIFA

# Serikali kutenga bajeti huduma ya upasuaji, upandikizaji vifaa sikivu

**Na Christina Mwakangale**

SERIKALI imesema inatarajia kuanza kutenga bajeti kwa ajili ya huduma ya upasuaji na upandikizaji vifaa vya usikivu ili kuwapunguzia gharama wagonjwa wanaohitaji huduma hiyo, wengi wakiwa watoto.

Matibabu nje ya nchi kwa anayehitaji upasuaji na uwekaji vifaa hivyo ni takribani Sh. milioni 34.

Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alisema hayo jana, jijini Dar es Salaam, wakati akizindua maabara ya kisasa na kituo cha upandikizaji vifaa vya usikivu pamoja na utoaji mafunzo bobezi Afrika kilichojengwa kwa Sh. bilioni 600 kwa kushirikiana na taasisi ya MED-EL ya Austria.

Alisema kituo hicho ambacho kimezinduliwa kwenye Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), kitaongeza umahiri kwa wataalamu wa ndani na nje ya nchi pamoja na kupanua wigo wa huduma kwa wagonjwa.

"Tunahitaji kutenga bajeti kwa ajili ya huduma hii kwa sababu gharama ni kubwa. Mtu mmoja gharama yake ni fedha nyingi ambayo wengi hawaimudu. Maabara ya kisasa kwa ajili ya kupandikiza wagonjwa wa sikio itakuwa na vitu sita.

"Kituo hiki kitafanya upasuaji na kuwekewa kifaa na kituo cha kibingwa bobezi kwa ukanda wa Kusini mwa Jangwa la Sahara. Maabara hii itajenga uwezo wa wataalamu wetu na tayari imefanya huduma kwa wagonjwa 58," alisema Prof. Makubi.

Alisema gharama hiyo ya Sh. bilioni 600 ni kutokana na uwekezaji wa kituo hicho na utoaji mafunzo kwa wataalamu kutoka nchi za ukanda huo, yatakayoanza mwaka huu hadi mwaka 2026.

Kaimu Mkurugenzi Mtendaji wa MNH, Dk. Rachel Mhavile, alisema maabara hiyo itawezesha wataalamu kuongezeka nchini na kuwafikia watu wengi, kwa kuwa kwa sasa kuna changamoto ya uhaba wa wataalamu, gharama kubwa ya vifaa vya usikivu ambayo mtu mmoja ni dola 15,000 (takribani Sh mil 34).

"Lengo ni kuwafikia watu wengi ila wengi hawamudu gharama. Watakapopata wataalamu wengi mafunzo itakuwa rahisi kupanua wigo wa huduma hii ambayo ni ya kibingwa," alisema Dk. Mhavile.

Awali, Dk. Mhavile alisema kutokana na gharama kuwa kubwa, wanaiomba Serikali kutenga bajeti ambayo itasaidia wagonjwa wengi kufikiwa na huduma hiyo wanaotoka maeneo tofauti.

Daktari Bingwa wa Masikio, Pia na Koo (ENT), Dk. Aslam Nkya, alisema gharama kwa mtoto mmoja ni Sh. milioni 45 na ikijumuishwa na gharama za anayemhudumia iwapo watakwenda nje ya nchi kama India, inafikia Sh. milioni 120. "Asilimia 80 ya watoto wanaopata tatizo la kuzaliwa nalo la usikivu wako Kusini mwa Jangwa la Sahara na kati yao asilimia tano pekee wamefikiwa na kutopata huduma inasababisha uziwi," alisema Dk. Nkya.

"Wataalamu sasa wako watatu wamesoma nje na hawa wanahudumia watu 25. Ndio maana wengine wawili wanakwenda nje kuongeza utaalamu. Sababu baada ya upandikizaji inahitajika wapatiwe kliniki hasa watoto, ikumbukwe mtoto ambaye hajawahi kusikia lazima afanyiwe ' rehabilitation'," aliongeza.



Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Ufundi na Umeme Tanzania (TAMESA), Lazaro Kilahala (kulia) akibadilishana mkataba na Meneja wa Kampuni ya African Marine, Sabeesan Asokan, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ukarabati wa kivuko cha MV Magogoni, jijini Dar es Salaam juzi. Anayeshuhudia (katikati) ni Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Prof. Makame Mbarawa. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

## TAKUKURU yabaini shule 36 hazina hati miliki

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Morogoro imebaini upungufu katika miradi minne ya ujenzi wa vyumba vya madarasa kwa ajili ya kupokea wanafunzi wa kidato cha kwanza mwaka huu, ikiwamo shule 36 za Halmashauri ya Morogoro kutokuwa na hati miliki.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Kaimu Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, Christopher Mwakajinga alisema upungufu huo ulibainika wakati wa ukaguzi uliofanyika kwa kipindi cha miezi mitatu kutoka mwezi Oktoba hadi Desemba 2022

Alisema katika kipindi hicho, taasisi hiyo ilifuatilia miradi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 175 yenye thamani ya Sh. bilioni 3.5 kwa ajili ya wanafunzi waliojiunga na sekondari mwaka huu.

"Katika ujenzi wa madarasa kwenye shule 36 za sekondari Halmashauri ya Morogoro wenye thamani ya Sh. milioni 720, shule zote zilizokaguliwa hazina hati miliki, pia baadhi ya majengo yaliongezwa ofisi kupitia fedha za halmashauri pamoja na zenye darasa moja, hazikufanyiwa marekebisho ya michoro ili kuendana na uhalisia wa ujenzi," alisema.

Aliongeza kuwa katika ujenzi wa vyumba 80 vya madarasa Manispaa ya Morogoro wenye thamani ya Sh. bilioni 1.6 nazo baadhi ya majengo yaliongezwa ofisi kupitia fedha za halmashauri pamoja na zenye darasa moja hazikufanyiwa marekebisho ya michoro ili kuendana na uhalisia wa ujenzi huku baadhi ya shule zikiwa hazina hati miliki.

Aliongeza kuwa upungufu mwngine ni katika ujenzi wa madarasa 30 yenye thamani ya Sh. milioni 600 wilayani Mvomero, kuwapo kwa maelekezo toka kwa viongozi juu ya bei elekezi tofauti na bei ya soko pamoja na kutozingatiwa gharama za vifaa vya ujenzi kwenye BOQ.

"Tayari tumeshatoa maelekezo halmashauri zote wafuate taratibu za hati miliki kwa shule zisizokuwa nazo ili kuepuka wananchi kuingia kwenye maeneo ya shule kinyume cha sheria, pia wahandisi wote tumewashauri kubadilisha michoro kwa shule zote zilizoongezwa ofisi," alisema.

Aliwakumbusha watendaji wote wa serikali kufuata taratibu zinazostahili kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za kuomba kubadilisha matumizi ya fedha ambazo zimekuwa zikibaki baada ya miradi mbalimbali kukamilika.

# Wanaharakati washauri jambo mchakato mabadiliko ya sheria

**Na Christina Mwakangale**

WADAU wa sheria na watetezi wa haki za binadamu wametoa maoni tofauti kuhusu hatua ya Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania, kuanza kukusanya maoni ya mapitio ya sheria mbalimbali, wakiweka angalizo kwamba mchakato huo uguse sekta na makundi yote nchini.

Wakizungumza kwa nyakati tofauti juzi, wadau hao wakiwamo Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC) na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), walisema kwa kuwa sheria nyingi zimepitwa na wakati, upatikanaji wa Katiba mpya ndio msingi.

Mratibu wa THRDC, Onesmo Olengurumwa, alisema kutokana na tume hiyo kuona jambo hilo ni la muhimu sasa, ipo haja kuwapo mchakato wa Katiba mpya, ili iwe msingi wa mabadiliko ya sheria zote.

"Kimsingi tunashukuru jitihada zinazofanyika kwa sababu sheria nyingi zina changamoto katika taifa letu, nyingi zimepitwa na wakati, pia tunahitaji kutengeneza sheria zingine.

"Mambo pia yamebadilika kiuchumi, kijamii, kisiasa, kiteknolojia tunahitaji kufanya mabadiliko ya sheria karibu zote, tutashiriki kwa nguvu zaidi, ili zifanyiwe kazi," alisema Olengurumwa.

Alisema kwamba tume hiyo inaposimamia mchakato huo, ijitahidi kufikia makundi yote kwenye sekta mbalimbali kama vile asasi za kiraia, haki za binadamu, mifugo, kilimo na uvuvi.

"Makundi hayo ndiyo yanajua changamoto ya sheria zao. Ila ili kuepuka kurekebisha sheria nyingi kwa wakati mmoja, tujitahidi kupata katiba mpya, ili zitakazorekebishwa ziendane na katiba mpya," aliongeza Olengurumwa.

Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema tume hiyo inapoanza mchakato huo, bado kuna changamoto kutokana na lengo kutowekwa wazi, kwa kuwa mara kadhaa wataalamu wa sheria wamekuwa wakichambua na kutoa maoni.

"Hatujui lengo hasa ni nani, tumekuwa tukichambua sheria nyingi tu na kutoa mapendekezo, kama kulikuwa na rekodi tunazo wangesema leteni tuone rekodi ambazo ni za kurekebishwa.

"Lakini kwa mwananchi wa kawaida ukimwambia ni sheria gani ina mapungufu anaweza asijue, kama wangeweka iwe nyepesi ni kero gani ipo kwenye jamii, labda mgambo wanatufukuza, wanachukua chakula, tungejua hii inahusiana na mipango miji," alisema Henga.

Alisema kwa uhalisia wananchi walio wengi hawawezi kuingia kwenye mfumo wa tovuti na kuelezea sheria zilizo na mahitaji ya kufanyiwa marekebisho.

"Sisi kama wataalamu tutapeleka tena, ila sidhani kama wananchi watashiriki, kutokana na ilivyowekwa kiugumu namna hii," alisema Anna.

Juzi, tume hiyo kupitia taarifa yao, ilisema, lengo la hatua hiyo ni kuhakikisha Tanzania, inakuwa na sheria zinazoendana na wakati kwa maendeleo endelevu, kutokana na sheria hizo kugusa maeneo mbalimbali.

Ilisema maandalizi ya Mpango wa Mapitio ya Sheria mbalimbali wa mwaka 2023-2025 yameanza na kuwaalika wananchi na wadau wote wa sheria kutoa maoni ya maeneo ya sheria husika, yanayoweza kuzingatiwa katika mpango huo.

Taarifa ya tume hiyo ilisema, ili kuwezesha upatikanaji wa maoni hayo, limendaliwa dodoso linalopatikana kwenye tovuti ya tume ambayo ni www.lrct.go.tz kutoa fursa kwa watu wote.

"Maoni yanaweza kuwasilishwa pia kwa Katibu Mtendaji wa Tume, kwa njia ya barua kupitia anuani ya hapo juu. Mwisho wa kupokea maoni ni tarehe 15 Machi, 2023," ilisema taarifa hiyo ya tume.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Hongera Rais Samia kwa kuhamasisha ushindi CAF

**BAADA** ya wawakilishi wa nchi waliobakia katika mashindano ya kimataifa yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba na Yanga zote za jijini, Dar es Salaam kuanza vibaya kwenye hatua ya makundi, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dk. Samia Suluhu Hassan ametoa ahadi ya fedha ili kuchagiza timu hizo kupata ushindi.

Simba inayoshiriki mashindano ya Ligi ya Mabingwa Afrika leo inawakaribisha Raja Casablanca kutoka Morocco, lakini itashuka dimbani kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa ikiwa na kumbukumbu ya kufungwa bao 1-0 na wenyeji wake, Horoya AC ya Guinea.

Mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga ambao wanashiriki katika michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika kesho watawaalika TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), wao walichapwa magoli 2-0 walipowafuata US Monastir ya Tunisia.

Kwa matokeo hayo, Simba na Yanga zinahitaji kupata matokeo chanya ili kurejesha ari ya kufikia malengo ya kufanya vizuri katika michuano hiyo inayofanyika kila mwaka hapa Afrika.

Rais Samia ametangaza kununua kila goli litakalofungwa na wachezaji wa timu hizo kwa Sh. milioni tano. Na anataka kuona magoli mengi yanafungwa katika mechi hizo mbili ambazo zinasubiriwa kwa hamu na mashabiki wa soka nchini ambao waliumizwa na matokeo ya michezo iliyopita.

Ahadi ya kiongozi huyo mkuu wa nchi inatakiwa ifanyiwe kazi na wachezaji, makocha pamoja na viongozi kwa kila mmoja kufanya vyema majukumu yake ili kupata ushindi na hatimaye kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele.

Kwa kufanya hivyo, Rais Samia ameonyesha kushiriki katika kuwaongezea hamasa wachezaji na wafahamu yuko pamoja nao katika kuhakikisha wanatekeleza vizuri majukumu waliyopewa.

Tunapenda kumpongeza Rais Samia kwa hatua hii aliyoichukua, kwa sababu anataka kuona wachezaji wanapambana kwa ajili ya kuipa heshima Tanzania ambayo kwa muda mrefu timu zake zimeonekana kuwa wasindikizaji kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

Huu ni wakati muhimu wa wachezaji wa Simba na Yanga kumpa heshima kubwa Rais Samia ambaye tangu ameingia madarakani, serikali yake imehakikisha wanamichezo mbalimbali wanaandaliwa vyema ili kwenda kuchuana katika mashindano ya kimataifa.

Tunawakumbusha ushindi katika mechi za nyumbani kutawaweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele huku tukiwataka wachezaji kuacha tabia ya kuzihofia timu za Waarabu. Wachezaji wanatakiwa wajiamini wanaweza kupata ushindi hata wanapokuwa ugenini, kikubwa ni kucheza kwa tahadhari na kuongeza umakini.

Wachezaji na makocha wanatakiwa kukumbuka kizuri hujiuza, matokeo au kiwango kizuri kitakachoonyeshwa katika mechi za wikendi hii zinaweza kuwafungulia milango ya kupata ofa nono zaidi kwa timu za ndani na nje ya Tanzania.

Wachezaji wanatakiwa kujituma ili kujiongezea thamani, kwa sababu kupitia michuano hiyo, mawakala kutoka nchi mbalimbali za Afrika na Ulaya hufuatilia, hivyo ni sehemu nyingine ya wao kujiweka sokoni kuzivutia klabu za nje na hatimaye kuwasajili.

Simba na Yanga, hakikisheni mnapambana na kumpa heshima Rais Samia ambaye ameamua kuongoza hamasa kuelekea mechi hizi muhimu za kimataifa.

Ili kufikia malengo, mashabiki wa soka nchini mnatakiwa pia kujitokeza kwa wingi katika mechi zote mbili, tukiweka pembeni upinzani wetu wa jadi kwa kuombeana dua njema na kuweka uzalendo mbele.

Kila la heri Wekundu wa Msimbazi, Kila la heri Yanga katika mechi za CAF. Kazi iendelee.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Simba, Yanga hizi ni mechi za kuonyesha uwezo wenu

Na Adam Fungamwango

**LEO** na kesho, mashabiki wa soka Tanzania wanatarajia kushuhudia mechi nzuri na ngumu za kimataifa, wakati wawakilishi kwenye michuano hiyo, Simba na Yanga zitakapokuwa uwanjani.

Kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, leo Simba itacheza dhidi ya Raja Casablanca ya Morocco ukiwa ni mchezo wa pili wa Kundi C, Ligi ya Mabingwa Afrika.

Simba itacheza mechi hiyo baada ya kuchapwa bao 1-0 ugenini Jumamosi iliyopita nchini Guinea, wakati Raja Casablanca ilishinda mabao 5-0 ikiwa nyumbani Morocco dhidi ya Vipers ya Uganda.

Kesho kwenye uwanja huo huo, Mabingwa wa Tanzania Bara, Yanga watashuka kuwavaa TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo kwenye mechi ya pili ya Kombe la Shirikisho barani Afrika.

Yanga ilipoteza mechi ya kwanza kwa kuchapwa mabao 2-0 Jumapili iliyopita ugenini dhidi ya US Monastir, huku TP Mazembe ilipata ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Real Bamako.

Pamoja na kuzitakia kila lakheri timu zote za Tanzania, lakini napenda tu niseme kuwa hizi ndizo mechi ambazo wanapaswa kuwaonyesha wanachama na mashabiki wao kuwa timu zao ni nzuri, na zina wachezaji wa viwango vya juu.

Kumekuwa na maneno mengi wakati wa usajili kuwapamba wachezaji hasa wa kigeni kwa sifa mbalimbali, ambazo wanakuja kuzitumia kwenye mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Kwa maoni na mawazo yangu binafsi, bado sijashawishika kuziona timu hizi ni bora na imara kwenye mechi za Ligi Kuu.

Ligi yetu ina mambo mengi ambayo yanafikirisha. Kwanza kabisa kuwa waamuzi ambao wakati mwingine, pamoja na makosa yao yanayotajwa kuwa ni ya kibinadamu, lakini wanatia shaka.

Kwa sababu mara nyingi makosa yao yanayotajwa ya kibinadamu, huzinufaisha timu hizo kongwe. Timu ndogo kwenye ligi pamoja na kujitutumua na wachezaji wao wa kawaida tu, lakini inafika wakati wanafelishwa na waamuzi wanaokuwa wanazibeba timu hizo zenye wachezaji wanaotajwa kuwa ni bora kutoka nje ya nchi na kulipwa mapesa mengi.

Kwa asilimia zaidi ya 80 kwenye ligi ya nchi hii bado inaznufaisha Simba na Yanga, kwani ukiondoa hilo la waamuzi, lakini zenyewe hazichezi saa nane mchana kwenye mechi zao.

Ukiacha hilo, hata kwa upande wa miundombinu na usafiri, Simba inaweza kwenda kucheza na Geita Gold uwanja wa CCM Mwanza, wachezaji wake wanapanda ndege kwenda huko, lakini wenyeji wanatoka Lindi baada ya kumaliza mechi yao dhidi ya Namungo, wanasafiri kwa barabara kwenda Mwanza kuiwahi mechi.

Matokeo yake mgeni anakuwa mwenyeji. Wachezaji wanafika wakiwa wamechoka sana. Inakuwa ni faida kwa Simba. Yanga nayo inakwenda Uwanja wa Sokoine kucheza dhidi ya Mbeya City kwa usafiri wa ndege, ikifika hapo wenyeji wao wanakuwa bado wapo njiani kutoka mkoani Kagera ilikuwa imekwenda kucheza dhidi ya Kagera Sugar. Wakifika hako hoi, hawapumziki wanaingia uwanjani bila hata kufanya mazoezi.

Haya ni baadhi ya mambo yanayofanya Simba na Yanga zipate kipimo sahihi cha upinzani kwenye ligi yetu. Ndiyo maana zinatamba tu kila kukicha. Zinashinda mfululizo, huku mashabiki wakitamba kuwa wana vikosi bora sana Afrika.

Sasa mechi hizi ni kipimo sahihi cha kuweza kujua uwezo halisi wa timu hizi. Ni kwa sababu kwenye ligi zinaweza kupata nafasi za kufunga zaidi ya mara 10 na kupata mabao mawili au matatu. Kwenye michuano ya kimataifa hakuna kitu kama hicho. Kuna wachezaji bora ambao hawakupi nafasi hizo, na hawafanyi makosa ya kizembe.

Huku tunaona, beki anajifunga mwenyewe mpira ambao anaweza kabisaa kuondoa, au kipa anampasia straika wa timu pinzani kwa namna ya kizembe, kitu ambacho kwenye mechi hizi hakuna.

Huku kutengeneza nafasi ni tabu mno. Zinaweza kupatikana nafasi nne tu au pungufu ya hizo kwenye mchezo mmoja kutegemea na timu unayocheza nayo.

**HABARI KITAIFA**

# Shaka akemea vinara migogoro ardhi

**Na Frank Kaundula,**
MOROGORO

MKUU wa Wilaya ya Kilosa mkoani Morogoro, Shaka Hamdu Shaka, amekemea baadhi ya watumishi ambao wamekua sio waadilifu Kwa kuendekeza rushwa jambo ambalo linachangia kuongezeka kwa migogoro ya ardhi wilayani humo.

Shaka aliyasema hayo jana katika Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa, baada ya kubaini baadhi ya watendaji wa vijiji na kata, madiwani na watumishi wengine ambao wamekuwa kikwanzo kwa serikali kukomesha changamoto hiyo kwa kuchukua rushwa kutoka kwa wafugaji na wakulima wahalifu.

Alisema katika uongozi wake hatakubali kumvumilia kiongozi ambaye atakuwa chanzo cha migogoro kwa kuendekeza rushwa na kuahidi kumshughulikia mtu yeyote atakayebainika kujihusisha na vitendo hivyo.

Mkuu wa wilaya alisema kwa kipindi kifupi alichokaa Kilosa, malalamiko mengi yanayoletwa na wananchi yanasababishwa na kukosekana kwa uadilifu wa viongozi kinyume cha taratibu za kimaadili.

"Nimekaa muda mfupi wa wiki mbili hapa Kilosa, nimegundua migogoro ya ardhi inasababishwa na viongozi kukosa uadilifu na uzalendo kwa kuendekeza vitendo vya rushwa, hivyo sitamvumilia mtendaji atakayekuwa kikwazo," alisema Shaka.

Shaka pia aliwataka watendaji kubuni vyanzo vya mapato na usimamizi bora wa ukusanyaji huku akikemea matumizi holela ya fedha mbichi na kutaka fedha zote ziingizwe benki ndipo zipangiwe matumizi.

Mwenyekiti wa Halmashauri Wilaya ya Kilosa, Wilfred Sumari, alisema kinachoendelea ni uzembe kwa sababu tayari serikali ya wilaya ilishatoa maelekezo kila kijiji kufanyike utambuzi wa mifugo.

Alisema ni muda mwafaka sasa kwa watumishi kuanza kuchukuliwa hatua kwa kuwa ndio wamekuwa chanzo cha tatizo hilo kwa kushindwa kutekeleza maagizo ya viongozi wa juu na kusababisha wilaya kuendelea kushamiri kwa migogoro.

"Tayari wilaya ilishatoa maelekezo kufanyike utambuzi wa mifugo na wafugaji na kuunda kamati za usuluhishi na kuondoa mifugo ambayo imeingia bila kibali, lakini baadhi viongozi wa kata wamekaidi maagizo hayo na kushindwa kutekeleza kwa makusudi," alisema.




Waziri wa Uwekezaji, Biashara na Viwanda, Dk. Ashatu Kijaji (kushoto), akijadiliana jambo na Naibu Balozi wa Ufaransa nchini, Axel-David Guillon (kulia) na Naibu Balozi wa EU nchini, Emilio Rossetti, baada ya mkutano wa waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu kongamano la uwekezaji kati ya Umoja wa nchi za Ulaya na Tanzania 2023, linalotarajiwa kufanyika Alhamisi na Ijumaa ya wiki ijayo, lenye malengo ya kuwaunganisha wawekezaji wa nje na wafanyabiashara wa ndani ili kubadilishana uzoefu na kushirikiana na watoa maamuzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bil. 31/- kuendeleza uchumi wa bluu

**Na Beatrice Shayo**

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega, amesema zaidi ya Sh. bilioni 11.5 zimetengwa kwa ajili ya kutengeneza boti za kisasa za uvuvi na Sh. bilioni 20 za ujenzi wa vizimba vya kufugia samaki aina ya sato kwenye Ziwa Victoria, ili kukuza uchumi wa bluu.

Aliyasema hayo juzi wakati wa ziara mkoani Tanga kutembelea vikundi vya ushirika vya ukuzaji viumbe maji vya Jifute, Mondura na Mchukuuni vinavyojishughulisha na ufugaji wa tango bahari pamoja na ukulima wa mwani.

Kwa mujibu wa Ulega, pia zimetengwa Sh. bilioni 2.5 za kuendeleza zao la mwani na kwamba Sh. milioni 447 zimeshatolewa kwa vikundi mbalimbali nchini.

Alisema serikali imejizatiti kuinua uchumi wa buluu kwa kutenga fedha nyingi huku wadau mbalimbali wa sekta hiyo wakikaribishwa kuunga mkono juhudi za Rais za kuweka mazingira mazuri ya ukuzaji viumbe maji.

"Serikali imeendelea kutekeleza bajeti ya mwaka wa fedha 2022/23 katika uwekezaji wa uchumi wa buluu kupitia maji ya Bahari ya Hindi, maziwa na mito ikiwemo kuhamasisha ufugaji wa viumbe maji," alisema Ulega.

Pia aliwataka wadau wa sekta ya uvuvi hususan vikundi vya ushirika vya wavuvi kuchangamkia fursa ambayo serikali imetoa fedha, ili kuongeza mahitaji ya ukuzaji viumbe maji kutokana na masoko yaliyopo ndani na nje ya nchi.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Pangani, Zainabu Abdallah alisema anafurahishwa na namna serikali inavyoweka juhudi za kuwasaidia vijana katika uwekezaji kwenye viumbe maji kupitia Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kutaka uwekezaji wa kisasa kwa kuongeza mnyoyoro wa thamani.

Alisema wameshatenga maeneo mengi kwa ajili ya shughuli za ukuzaji viumbe maji.

Akisoma risala ya Kikundi cha Ushirika cha Kilimo cha Mwani na Ufugaji Tango Bahari Mchukuuni jijini Tanga, Abdallah Mtondo alilalamikia baadhi ya watu wasio waaminifu kuiba matango yaji yanapofunika mashamba yao.

Mtondo aliiomba serikali kuwachukulia hatua za kisheria watu hao ambao wamekuwa wakiwarudisha nyuma kwenye shughuli za ufugaji, ili kujiongezea tija.

Ulega alilitolea jambo hilo kauli kali na kutaka mamlaka husika kuingilia kati jambo hilo huku akisisitiza wanunuzi wa mwani na tango bahari kununua mazao hayo kwenye vikundi vinavyotambulika na kusajiliwa.

## Mahakama yazuia CCM, wizara kuendeleza eneo

**Na Kulwa Mzee**

BODI ya Wadhamini ya CCM, Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na wadau wengine wamezuiwa kufanya shughuli zozote za ujenzi katika eneo lenye mgogoro kati yao na Kanisa Katoliki wilayani Uvinza hadi kesi itapomalizika.

Amri hiyo ya zuio ilitolewa juzi na Mahakama Kuu Kanda ya Kigoma mbele ya Jaji Mfawidhi, Lameck Mlacha, baada ya Kanisa Katoliki kuwasilisha maombi wakidai CCM wanataka kupewa eneo lao.

Kanisa Katoliki Jimbo la Kigoma liliwasilisha maombi chini ya hati ya dharura likidai ni wamiliki wa eneo hilo lililoko Nyambutwe, wilayani Uvinza.

Mleta maombi katika shauri hilo, anawakilishwa na Wakili Method Kabuguzi akishirikiana na Wakili Mgaya Mtaki na wajibu maombi wanawakilishwa na Fabias Donatus na Hamis Kimilomilo huku upande wa Serikali ukiwakilishwa na Wakili Allan Shija.

Waombaji katika shauri hilo wanadai mjibu maombi namba mbili wizara na Halmashauri ya Uvinza wamepanga kuchukua eneo lao kuwapa CCM bila ridhaa yao kwa ajili ya kujenga madarasa ya Shule ya Sekondari ya Chumvi.

Kanisa Katoliki liliiomba mahakama kukubali kutoa amri ya zuio la muda kwa wajibu maombi na mawakala wao au watu wengine kujenga au kuendeleza eneo hilo lenye ukubwa wa ekari 39.6.

Baada ya kusikiliza maombi hayo mahakama iliyakubali na kutoa amri tatu kwamba kuanzia jana CCM na wengine wote kwenye eneo lenye mgogoro hawaruhusiwi kujenga ama kuendeleza kitu chochote mpaka kesi itakaposikilizwa na kuamriwa.

Mahakama imezuia upande wa serikali kufanya ama kuendelea na upimaji katika eneo lenye mgogoro. Pia serikali hairuhusiwi kufanya ugawaji ama umilikishaji wowote kwenye eneo lenye mgogoro.

Upande wa serikali uliwasilisha majibu ya madai yanayowakabili lakini CCM walikuwa hawana majibu yoyote waliomba wapewe muda hivyo mahakama iliwaamuru kuwasilisha majibu yao ndani ya siku saba.

Awali, Wakili wa CCM, Fabian Donatus alidai nyaraka zilihifadhiwa katika ofisi ya Kigoma na kwa bahati mbaya zilichelewa kuwafikia Dodoma hivyo wakaomba siku saba, ili kuweza kuwasilisha majibu ya kiapo kinzani na kuendelea na kesi hiyo.

Wakili wa Mleta maombi, Mgaya Mtaki alidai ni haki yao ya msingi kuwasilisha hati ya kiapo kinzani mahakamani hapo wao hawana pingamizi. Aidha, mahakama hiyo imepanga kuendelea na shauri hilo Machi 3, mwaka huu.

Shauri liliwasilishwa chini ya hati ya dharura na kupewa namba 42/2022 dhidi ya Bodi ya Wadhamini ya CCM, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Halmashauri ya Wilaya ya Uvinza na Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

# DC awaweka kikaangoni viongozi waliokacha kikao tathmini elimu

**Na Steven William,**
NACHINGWEA

MKUU wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi, Mohamed Moyo amewaita viongozi wote ofisini kwake ambao hawajahudhuria kikao cha tathmini ya elimu wilayani hapo ili wajieleze.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa kikao hicho kilichokuwa mahususi kujadili masuala ya elimu kilichowashirikisha viongozi mbalimbali wa wilaya na wadau wa sekta hiyo.

Moyo alisema anawaita viongozi wote ofisini kwake ambao hawajahudhuria kikao hicho ambacho kilikuwa na lengo la kujua changamoto za elimu na kuzipatia ufumbuzi ili kujua sababu za kutokuhudhuria kwao. Alisema viongozi hao wanapaswa kufika ofisini kwake mara moja.

Licha ya kuwataka waliokacha kikao hicho kuripoti na kujieleza kabla ya kuchukuliwa hatua, Moyo aliwataka viongozi katika ngazi mbalimbali wilayani hapa kuongeza ubunifu wa namna ya kuongeza ufaulu kwa wanafunzi na kuifuta kabisa alama sifuri kwenye matokeo ya mitihani mbalimbali.

Moyo alisema hataki kusikia mwanafunzi amepata alama sifuri kwenye matokeo yoyote yale katika wilaya ya Nachingwea.

Alisema ameangalia kwa miaka mitatu hadi minne ya nyuma na sasa bado hali ya ufaulu iko chini, hivyo walimu na viongozi lazima waongeze maarifa ya kufundisha wanafunzi ili kuongeza ufaulu na kufuta kabisa sifuri.

Mkuu huyo alisema ametoka katika wilaya ya Iringa ambayo imekuwa ikishika nafasi za juu za ufaulu kila mwaka, hivyo hataki kusikia Nachingwea inashika nafasi ya mwisho bali juhudi ziongezeke ili kuongeza ufaulu kwa wanafunzi.

"Nimekuja hapa nikiwa na maono ya kukuza elimu ndani ya wilaya ya Nachingwea. Sitaki mchezo kwenye elimu, hivyo mtu yoyote yule atakayechezea sekta ya elimu atapata haki yake," alisema Moyo.



Mkurugenzi wa Huduma za Tiba wa Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo (wa tatu kulia) akipata maelezo kutoka kwa Mwenyekiti wa Chama cha watengenezaji wa dawa tiba nchini (TPMA) Bashir Haroon (kulia), alipotembelea maonyesho ya 24 ya dawa na vifaa tiba vya afya, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Waombwa kuwekeza katika sekta ya afya

**Na Halfani Chusi**

SERIKALI imefungua milango kwa wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kwenye sekta ya afya ili kujiimarisha zaidi kwenye eneo hilo kutokana na kuwapo kwa ongezeko la wagonjwa wanaotoka nchi jirani kutibiwa Tanzania.

Mkurugenzi wa Huduma za Tiba kutoka Wizara ya Afya, Prof. Paschal Ruggajo, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizindua Maonyesha ya 24 Medexpo Africa, yatakayofanyika kwa siku tatu kuanzia juzi.

Alisema maonyesho hayo ni muhimu kwa sababu yamezikutanisha zaidi ya kampuni 50 kutoka nchi mbalimbali kwa lengo la kuonyesha vifaa tiba, kinga, ugunduzi wa magonjwa mapema pamoja na vifaa vya maabara.

"Ni huduma muhimu kwa watu afya, wanaweza kuja kujifunza kutoka kwa wawakilishi wa kampuni kubwa na duniani na kubadilishana ujuzi.

"Ni fursa kwa sekta yetu ya afya ambayo inazidi kuimarika kila siku, nitoe wito kwa wafanyabiashara, wananchi pamoja na taasisi za afya kufika hapa ili kubadilishana uelewa na wataalamu waliokuja kwa ajili ya maonesho haya," alisema.

Mwenyekiti wa Chama cha Wawekezaji Viwanda vya Dawa Tanzania, Bashir Haroon, aliishukuru serikali kwa kuwakumbatia wawekezaji wanaowekeza kwenye sekta ya afya akisifia ushirikiano mzuri wanaopewa.

"Mwezi wa kwanza tulionana na Waziri wa Afya (Ummy Mwalimu) akatueleza nia njema ya serikali kutusaidia wawekezaji wenye nia ya kuwekeza kwenye sekta hii na sisi ni mashahidi serikali imekuwa ikitupa msaada mkubwa kila tunapohitaji," alisema.

Mratibu wa Maonyesho hayo kutoka Expogroup, Duncan Njage, aliwataka Watanzania kufika eneo hilo na kupata uelewa zaidi juu ya masuala ya afya.

# Waziri ataka bodi chuo kuwa wabunifu wa vyanzo vya mapato

**Na Munir Shemweta,**
MOROGORO

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, ameitaka Bodi ya Chuo cha Ardhi Morogoro (ARIMO) kuwa wabunifu wa vyanzo vya mapato na kuweka msukumo kuhakikisha chuo kinafanikiwa katika kutekeleza majukumu yake kisheria.

Pia ameitaka bodi kuhakikisha inapata taarifa kuhusiana na fedha za mkopo wa riba nafuu iliyopatiwa kwa ajili ya kazi za urasimishaji makazi holela ili mkopo huo urudishwe kwa wakati.

Dk. Mabula alisema hayo juzi wakati akizindua bodi mpya ya ARIMO katika hafla iliyofanyika chuoni hapo.

Bodi mpya ya ARIMO inaongozwa na Balozi Job Masima na imeanza kazi Febriari Mosi, mwaka huu na itafikia ukomo Januari 31, 2026.

Kwa mujibu wa Dk. Mabula, katika mwaka wa fedha 2020/21 na 2022/23, Wizara ilikipatia chuo mkopo usio na riba wa Sh. bilioni 1.273 zilizotumika katika utekelezaji wa mradi wa urasimishaji makazi katika mji wa Mbalizi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

alisema wizara yake imekuwa ikikisaidia chuo katika masuala mbalimbali kama vile kukipatia msaada wa vifaa vya kisasa vya upimaji kwa ajili ya kufundisha na kutekeleza miradi mbalimbali.

"Wizara itaendelea kukisaidia chuo katika kuboresha miundombinu kupitia mradi wa uboreshaji usalama wa milki za ardhi. Mradi huu ni vizuri ukatumika kama fursa ya wanafunzi kujifunza kwa vitendo," alisema Dk. Mabula.

Aliukumbusha uongozi wa ARIMO katika kuwatumia wanafunzi kwenye miradi ya kupanga na kupima. Alisema pamoja na utaratibu huo kuwa mzuri kutokana na kuongeza umahiri kwa wanafunzi, utekelezaji wake unapaswa kuzingatia ratiba ya wanafunzi wakati wa kwenda uwandani.

"Chuo pamoja na kupata kazi kihakikishe kazi zitakazopatikana na zinazoendelea kufanyika, kufanya kwa mujibu wa malengo na kutekeleza kwa wakati na weledi ili mradi wasiharibu ratiba ya chuo," alisema.

Waziri pia aliutaka uongozi wa chuo kuchukua kazi katika maeneo ambayo itakuwa rahisi kusimamia bila kuvuruga ratiba za masomo.

Kaimu Makamu Mkuu wa ARIMO, Charles Saguda, alisema chuo kimeshiriki kikamilifu katika programu ya urasimishaji makazi nchini huku akibainisha kuwa kati ya mwaka 2016 na 2023, kimetekeleza miradi ya urasimishaji katika mitaa 80 iliyoko mikoa saba ya Arusha, Dar es Salaam, Iringa, Kilimanjaro, Mbeya, Morogoro na Mtwara.

"Katika mitaa tuliyotekeleza urasimishaji, jumla ya viwanja 67,646 (asilimia 65) vimeidhinishwa na kati ya viwanja 103,972 vilivyopimwa na viwanja vilivyosalia yaani 36,326 (asilimia 35) vina changamoto mbalimbali ambazo tunaendelea kuzishughulikia kwa kushirikiana na mamlaka za upangaji," alisema Saguda.

Pia alisema chuo kimefanikiwa kufanya upimaji katika maeneo mapya jijini Dodoma na Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino na kuongeza kuwa hivi karibuni chuo kimeingia mkataba na Shirika la Reli Tanzania (TRC) unaolenga kuweka miundombinu ya upimaji katika maeneo 26 ya reli kuandaa topografia, kupanga na kupima viwanja pamoja na kuweka alama za mipaka ya reli katika maeneo ya mradi.

Pamoja na mafanikio, Saguda alisema chuo kina uhaba wa watumishi hasa wakufunzi, vifaa vya kufundishia na miundombinu.

Mkurugenzi wa Utawala na Rasilimali Watu wa Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Sheushi Mburi, ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara, Dk. Allan Kijazi, alisema wizara itashirikiana na chuo kutatua changamoto zote ikiwamo uhaba wa watumishi.

Hata hivyo, alisema wakati mchakato wa kupata watumishi ukiendelea, chuo kinapaswa kuainisha watumishi walio katika taasisi zingine walio tayari kufundisha katika chuo hicho.





## Pinda ataka kuibaini mikoa vinara ukatili

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Mizengo Pinda ameishauri Jumuiya ya Maridhiano nchini kushirikiana na serikali kubaini mikoa ambayo inaongoza kwa vitendo vya ukatili ili kuweka nguvu kubwa ya kukabiliana navyo.

Pinda aliyasema hayo jijini hapa juzi alipokuwa akifungua kikao cha maandalizi ya siku ya maridhiano kitaifa yanayotarajiwa kufanyika Machi 3, mwaka huu. Rais Samia Suluhu Hassan anatarajiwa kuwa mgeni rasmi.

Alisema ukatili chimbuko lake ni ngazi ya familia, hivyo ni vyema jumuiya hiyo inapokutana na makundi mbalimbali kutoa elimu stahiki ya masuala ya ukatili. "Tuangalie maeneo ambayo vitendo hivyo vimekithiri ili kuweka nguvu ya ziada na mikakati ya kukabiliana. Pia katika shughuli mbalimbali mnazofanya zinazokusanya makundi mbalimbali, hakikisheni mnatoa elimu na kwa kufanya hivyo mtajikuta mmewafikia watu wengi kwa kipindi kifupi," alisema.

Sambamba na hilo, alimpongeza Rais Samia kwa kuendelea kudumisha amani, utulivu na mshikamano nchini.

Aliishukuru serikali kwa kuwa karibu na chombo hicho na kuhakikisha kinaendelea kufanya kazi kama ilivyokusudiwa ya kuimarisha amani na utulivu nchini.

Pinda ambaye pia ni mlezi wa jumuiya hiyo, alisema jumuiya hiyo ilitokana na mambo yaliyojitokeza na kazi kubwa ni kuzuia uvunjifu wa amani na utulivu kwa njia ya kukutana na jamii kwa kuzungumza na wananchi bila kungoja mifarakano itokee.

Alisema kuwa tangu kuanza kwa jumuiya hiyo wamepata faraja kwa sababu imekutanisha watu kutoka katika madhehebu mbalimbali na huu ndio moyo tulitaka ujengwe miongoni mwa Watanzania.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, Israel Maasa, alisema jumuiya hiyo kwa kipindi cha miaka miwili imeendelea kujiimarisha katika mikoa yote ya Tanzania bara na kuunganisha viongozi kutoka katika dini zote na kimila.

Alisema katika kipindi cha miaka miwili imeendelea kuunga mkono jitihada za serikali na kuhakikisha viongozi wa dini wanasimama na serikali katika kuhakikisha Watanzania

# Kasi ya uzazi vijijini yazidi kupaa

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

KIWANGO cha uzazi kwa Tanzania Bara, kiko juu zaidi maeneo ya vijijini kuliko mijini.

Ripoti ya utafiti wa afya ya uzazi na mtoto na viashiria vya malaria kwa mwaka 2022 iliyozinduliwa na Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, imebainisha kiwango hicho.

Katika ripoti hiyo iliyoandaliwa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS), kwa wastani, mwanamke wa kijijini anazaa watoto 5.5 katika maisha yake, ikilinganishwa na wastani wa watoto 3.6 kwa mwanamke wa mjini.

Utafiti huo umefanyika kwa wanawake wenye umri wa miaka 15-49 na kama kiwango cha sasa cha uzazi hakitabadilika, mwanamke nchini Tanzania anazaa wastani wa watoto 4.8 katika maisha yake.

Taarifa hiyo imebainisha kwamba kiwango cha uzazi ni kidogo zaidi miongoni mwa vijana (watoto 112 kwa kila wanawake 1,000 wenye umri wa miaka 15-19), kinaongezeka kufikia watoto 222 kwa kila wanawake 1,000 wenye umri wa miaka 25-29, na kisha kinapungua kadri umri wa mwanamke unavyoongezeka.

Kuhusu uhitaji wa kuzaa watoto, utafiti huo unaonyesha asilimia 24 ya wanawake wanahitaji mtoto mwingine karibuni (ndani ya miaka 2 baada ya kujifungua), asilimia 35 wanataka kupata mtoto mwingine baadaye (katika miaka 2 au zaidi) na asilimia mbili wanataka mtoto mwingine lakini hawajaamua ni lini wangetaka kupata mtoto.

Pia asilimia 23 ya wanawake wanasema hawahitaji watoto zaidi au wamefunga kizazi huku asilimia ya wanawake ambao hawahitajii watoto zaidi au waliofunga kizazi wameongezeka kwa idadi ya watoto walio hai kutoka asilimia moja ya wanawake ambao hawana watoto kulinganisha na asilimia 56 ya wanawake wenye watoto sita au zaidi.

Kuhusu matumizi ya uzazi wa mpango, asilimia 38 ya wanawake walioolewa kwa sasa wanatumia njia yoyote ya uzazi wa mpango, ikijumuisha asilimia 31 ya wanaotumia njia zozote za kisasa na asilimia saba ya wanawake wanaotumia njia za asili za uzazi wa mpango.

Njia ya vipandikizi ndiyo njia inayotumika zaidi miongoni mwa wanawake walioolewa (asilimia 14), ikifuatiwa na njia ya sindano (asilimia tisa).

Miongoni mwa wanawake wasioolewa lakini wanashiriki tendo la kujamiiana, asilimia 45 hutumia njia yoyote ya uzazi wa mpango, ikiwa ni pamoja na asilimia 36 kutumia njia yoyote ya kisasa na asilimia 8 kutumia njia yoyote ya asili.



Ofisa Habari wa Bunge, Halima Laizer akitoa elimu kuhusu masuala ya bunge kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari za Iyunga na Iwambi, jijini Mbeya jana. Wafanyakazi wa Bunge la Jamhuri ya Tanzania wapo kwenye ziara ya kutoa elimu ya masuala mbalimbali yanahusu muhimili huo kwa wanafunzi. **PICHA: BUNGE**

# Ndugai atoa neno usimamizi ujenzi shule

**Na Peter Mkwavila,**
KONGWA

SPIKA Mstaafu wa Bunge, Job Ndugai, amewataka wasimamizi wa mradi wa ujenzi wa nyumba za walimu katika Shule ya Sekondari Chitego kutumia fedha zilizotolewa na serikali kukamilisha bila kisingizio chochote.

Ndugai ambaye ni Mbunge wa Kongwa aliyasema hayo juzi alipokuwa akizungumza na wananchi wa Kata ya Chitego kwenye hafla ya uzinduzi wa ujenzi wa mradi wa nyumba za walimu wa shule hiyo wilayani hapa.

Mradi huo wenye thamani ya Sh. milioni 202, unatekelezwa na kusimamiwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) ikiwa ni kipaumbele walichoibua wakazi wa kata hiyo.

Ndugai alisema fedha zilizotolewa zinatosha kujenga hadi kukamilisha mradi huo kinachohitajika ni usimamizi na matumizi yaliyokusudiwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, White Zuberi, alisema wilaya imekuwa ikifanya vibaya katika matokeo ya mitihani ya taifa tatizo ambalo kimsingi linasababishwa na wazazi na si wanafunzi.

Alisema wako baadhi ya wazazi ambao wamekuwa wakiwageuza watoto wa kike kuwa kitegauchumi kwa kuwapeleka mijini hasa Dar es Salaam kufanya kazi za ndani kwa lengo la kujipatia kipato, hivyo kuitaka jamii kuwaheshimu watoto wa kike.

Mkurugenzi Mtendaji Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, Dk. Omary Nkullo, alisema haipendezi serikali kutumia fedha nyingi kuboresha miradi ya elimu lakini jamii inakuwa kikwazo cha ufanisi kwa kutochangamkia fursa za elimu kwa watoto wao huku wengine wakiwazuia kufanya vizuri mitihani ya taifa.

Awali, Mratibu wa TASAF Wilaya ya Kongwa, Elias Chilemu, alisema mradi unaotekelezwa utatumia Sh. milioni 202, ambazo kati yake wananchi watachangia nguvukazi yenye thamani ya Sh. milioni 12.39.

Katika hafla hiyo, Ndugai alikabidhi zaidi ya Sh. milioni 171 kwa ajili ya kutekeleza mradi huo wa ujenzi wa nyumba za walimu.





# Sera ya Taifa Uwezeshaji imezingatia uhamasishaji matumizi bidhaa za ndani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

SERA ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar ya Mwaka 2022 imezingatia uhamasishaji wa matumizi ya bidhaa za ndani pamoja na kuihuisha nembo za bidhaa za Zanzibar (Made in Zanzibar).

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu swali la Mwakilishi wa Mwanakwerekwe, Amer Abdallah.

Waziri huyo alisema katika kuhamasisha wananchi kuzithamini bidhaa zao za ndani, hakuna budi kuwa na ushirikiano wa wadau wote wakiwamo viongozi wa siasa na viongozi wengine katika ngazi zote kushiriki katika kuhamasisha matumizi ya bidhaa za ndani kupitia majukwaa yao na sehemu mbalimbali wanazozifikia.

"Pia tunaandaa vipindi maalum katika vyombo vyetu vya habari kwa ajili ya kutangaza na kuhamasisha utumiaji wa bidhaa za ndani," alisema.

Aliongeza kuwa wakala unawasaidia na kuwashajiisha wajasiriamali katika masuala ya kuimarisha ubora wa bidhaa ili kupata hati za ubora wa viwango nchini ili bidhaa ziwe na ushindani ulio sawa na bidhaa za nje.

Alisema suala la kuimarisha masoko kwa bidhaa za wajasiriamali ni kipaumbele kikubwa cha serikali na mikakati inaendelea kufanyiwa kazi.



Waziri wa Afya wa Zanzibar, Nassoro Mazrui (wa tatu kushoto), akipokea vifaa tiba kutoka kwa Mwakilishi Mkaazi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner, jijini Zanzibar juzi, vilivyotolewa na serikali ya Canada kupitia mradi wa Wezesha, unotekelezwa na UNFPA, kwa ajili kliniki ya huduma rafiki kwa vijana ya Bumbwini. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Sheria ya Mtoto kufumuliwa kukabili ukatili wa kijinsia

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Maendeleo ya Jamii Jinsia Wazee na Watoto imesema iko katika mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Mtoto Na. 6 ya Mwaka 2011 kwa lengo la kudhibiti matukio ya udhalilishaji, ikiwamo kutelekeza watoto na kuwatupa baada ya kuzaliwa.

Naibu Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Anna Athanas Paul alibainisha hayo jana wakati wa kikao cha Baraza la Wawakilishi alipojibu swali la Mwakilishi wa Viti Maalum (Wanawake) Mkoa wa Kusini Unguja, Salma Mussa Bilali.

Mwakilishi huyo alitaka kujua hatua zinazochukuliwa na serikali kukabiliana na matukio ya vitendo vya utupaji wa watoto mara tu baada ya kuzaliwa na wazazi wao.

Paul alisema serikali imesikitishwa na matukio ya wazazi kuwatupa watoto wao baada ya kuzaliwa, kitendo ambacho ni kinyume cha sheria na ni ukatili wa kutisha dhidi ya kundi hilo.

Alisema hivi karibuni kumejitokeza matukio ya aina hiyo ya wazazi kuwatupa watoto wao baada ya kuzaliwa huku wengine wakipoteza maisha na wengine kuokolewa na wasamaria wema.

Alibainisha kuwa kwa mwaka huu ambao una mwezi mmoja na nusu, tayari jumla ya matukio manne ya watoto wachanga kutupwa mara baada ya wazazi wao kujifungua yameripotiwa huku wengine wakipoteza maisha.

Alisema matukio ya utupaji wa watoto wachanga baada ya kuzaliwa hayakubaliki na ni ukatili ambao unakwenda kinyume cha sheria na ni kosa la jinai.

Alitoa mfano wa mtoto mchanga ambaye aliokotwa hivi karibuni akiwa ametupwa kwenye jaa huko Fuoni muda mfupi baada ya kuzaliwa huku kitovu chake kikitoka damu ikionyesha dhahiri alikuwa amezaliwa muda mfupi uliopita.

"Matukio ya kutupa watoto wachanga mara baada ya kuzaliwa hayakubaliki na ni kinyume cha maadili, mila na silka lakini pia ni kinyume cha Sheria ya Makosa ya Jinai ambapo kwa upande wa wizara tunawahakikishia watoto wa aina hiyo watapatiwa hifadhi ya kudumu kwa muda wote wa maisha yao," alisema.

Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Riziki Pembe Juma, alisema watoto wote wanaotupwa na kutekelezwa, wanapatiwa hifadhi ya kudumu kwenye nyumba ya wazee iliyoko Mazizini mjini Unguja.

Alisema baada ya Mapinduzi ya Januari 12, 1964, serikali chini ya Hayati Abeid Amani Karume, ilianzisha nyumba ya kuhifadhi watoto yatima kwa ajili ya kupata hifadhi ya kudumu baada ya kuondokewa kwa njia moja au nyingine wazazi wake.

# Wizara yaona fursa wanawake kujiendeleza kazi za mikono

**Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR**

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar imesema kuanzishwa kwa vyuo vya amali ni fursa nyingine muhimu kwa wanawake kujiendeleza kwa kazi za mikono na kujiajiri.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais - Kazi, Uchumi na Uwekezaji, Mudrik Ramadhan Soraga alitoa kauli hiyo jana alipojibu swali la Mwakilishi wa Pandani, Pemba, Prof. Omar Faki Hamad aliyetaka kujua idadi ya wanawake waliopatiwa ujuzi na kujiajiri tangu kuanzishwa kwa vyuo vya amali Zanzibar.

Soraga alisema takwimu zimebainisha kwamba tangu mwaka 2010 hadi 2022, jumla ya wanafunzi wa kike 3,190 sawa na asilimia 36, walisajiliwa katika fani mbalimbali zinazotolewa katika vyuo vya amali vilivyoko Unguja na Pemba.

Alisema kuwa kati ya wanafunzi 1,990, sawa na asilimia 62, walifanikiwa kumaliza masomo yao na kuutumia ujuzi wa maarifa ya mafunzo waliyopewa, kujiajiri katika sekta mbalimbali.

Pia alisema wizara yake iko katika matayarisho ya Sera ya Taifa ya Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi ya Mwaka 2022 ambayo imeweka mikakati katika masuala ya mafunzo, mitaji, masoko na miundombinu kwa wajasiriamali na wafanyabiashara wadogo kupiga hatua kubwa ya maendeleo.

Alisema mikakati yote hiyo itazingatia uwiano wa usawa wa kijinsia ili kuona kundi la wanawake linapata mafunzo yatakayowaingiza katika kazi za ujasiriamali.

"Kwa mfano, kuanzia Julai hadi Desemba mwaka 2022, jumla ya wajasiriamali 863 ambapo 453 ni wanawake, walipatiwa mafunzo juu ya mbinu za uzalishaji wa bidhaa mbalimbali kuingia kwenye masoko yakiwamo ya matunda na mboga.

Alisema serikali kupitia fedha za UVIKO-19, ilitenga jumla ya Sh. bilioni 37 kwa ajili ya kuwawezesha wajasiriamali wadogo kupiga hatua kubwa ya maendeleo na kuibua miradi ikiwamo ya uchumi wa bluu katika mazao ya baharini.

Alisema zipo fursa nyingi kwa wanawake katika mazao ya baharini ikiwamo kilimo cha mwani, ufugaji wa samaki na mazao ya matango bahari pamoja na kaa ambapo bei ya mazao hayo ipo juu kwenye soko la dunia.

"Mheshimiwa Naibu Spika, hiyo ndiyo mikakati yetu ya kuona kwamba kwa kiasi gani tunawanyanyua wanawake kupiga hatua kubwa za maendeleo na kujikomboa katika kuelekea kujitegemea," alisema.



**AKA**
UKURASA 12

Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
UDANI
TELE

JUMAMOSI FEBRUARI 18, 2023



# 'NA IWE KHERI'

KILA kukicha afadhali ya jana! Ndivyo inavyoonekana kwa wanamuziki wawili kutoka lebo ya WCB, Diamond Platnumz na Zuchu, ambao kila siku wanagonga vichwa vya habari kutokana na ukaribu wao.

Muda mrefu wawili hao wamekuwa wakihusishwa wanatoka kimapenzi, na hata maongezi yao yanaashiria kuwa kuna zaidi ya kazi kati yao.

Juzi Zuchu amewashtua watu baada katika ukurasa wake wa Instagram kuweka picha akionekana akiwa na Diamond huku wakiwa katika pozi la kimahaba na wakiwa katika vazi la kiheshima ambalo linatumika zaidi kwenye harusi za kiislam.

Licha ya kuonekana picha hiyo kuwa si ya kawaida, lakini wengi walioshiriki maoni kwenye picha hiyo walihoji kwa nini wasanii hao wasiweke wazi uhusiano wao, badala yake wanakuwa kama wafungwa.

Fununu za wanamuziki hao kuwa katika uhusiano wa kimapenzi limekuwa jambo la kawaida, lakini picha ya aina hiyo imetoka kwa mara ya kwanza na kuashiria pengine kuna jambo linataka kutokea linalowahusu wao.

Wanafamilia wa Diamond, walijitokeza kumpongeza ndugu yao, kama dada yake Asma, aliandika kwa kifupi kwa kumtaja Zuchu kama 'Bi harusi'.

Idd Santos ambaye ni kaka yake Diamond, aliandika "Na ikawe Kheri Angalau Tushapata Pakuftari", ujumbe ambao unaonekana na wengi kama ishara ya kuwepo kwa harusi kati ya wasanii hao.

BASI SAWA


## Mbosso anusurika kifo

MWANAMUZIKI nyota wa Bongo Fleva,kutoka lebo ya WCB, Mbosso amenusurika katika ajali iliyotokea nchini Marekani.

Mbosso kwa sasa anafanya ziara ya muziki nchini Marekani kutangaza albamu yake ya 'Definition of Love' na amefanikiwa kuwakonga nyoyo mashabiki wake nchini humo.

Kupitia Insta Story yake, Mbosso ameeleza kwamba amepata majeraha kwenye bega, mkono pamoja na uti wa mgongo, lakini hayuko katika hali mbaya.

Amewatoa hofu mashabiki zake kuwa yuko salama na anaendelea vizuri kwani baada ya ajali hiyo polisi walifika na kumuwahisha hospitali kupatiwa matibabu.



## Yobele, Wamwiduka wageukia asili

Baada ya kufanya vizuri kwenye muziki wa Injili, mwimbaji Deogratius Yobele, ameibukia katika muziki wa asili akishirikiana na msanii mwenzake Wamwiduka.



Akizungumza na gazeti hili mapema jana, Yobele amesema kwa sasa anafanya muziki unaoitwa Baba Toni ukiwa na vionjo vya asili ya Mbeya na kwa kuanza ametoa wimbo unaoitwa Wazazi.

"Wazazi ni aina tofauti ya muziki, unaitwa Baba Toni ambao umeandaliwa na ala za muziki za asili kutoka Mbeya, naamini kila mtu ataufurahia hasa ujumbe wake ambao unaonyesha umuhimu wa kuheshimu wazazi, wimbo utaanza kupatikana mtandaoni muda wowote kutoka sasa," amesema Yobele.




# AKA KUZIKWA KAWAIDA

BAADA ya Rais wa Afrika Kusini, Cyril Ramaphosa, kukataa ombi la kuyafanya mazishi ya rapa maarufu nchini humo, Kiernan Forbes, maarufu kama AKA, kuwa ya kitaifa sasa atazikwa kawaida. Awali Waziri Mkuu wa Gauteng, Panyaza Lesufi, alimwandikia Rais Ramaphosa, akiomba ruhusa ya kumpa rapa huyo aliyeuawa kwa kupigwa risasi hadhi ya mazishi ya kitaifa.

Katika ombi hilo, hakuomba fedha za serikali kwa ajili ya mazishi, bali jeneza lifunikwe bendera ya taifa na bendera kupeperushwa nusu mlingoti kwa heshima ya rapa huyo.

"Tulihisi kwamba mtu wa hadhi yake ya kimataifa, mtu wa hadhi ya kitaifa, lazima kuwe na aina fulani ya heshima, na tunataka kufafanua sio mchango wa kifedha," alinukuliwa akisema.



# Sultan King atamba 'Happy Valentine'

MWANAMUZIKI kutoka Zanzibar, Sultan King, amesema ngoma yake mpya 'Happy Valentine' inafungua upya tasnia ya muziki kisiwani humo.

Muimbaji huyo amesema kuwa wimbo huo ambao unawagusa wanaopendana, unatoa ujumbe kwamba yeye bado yupo na wakati wowote atangia rasmi kupambana na wakongwe.

"Wimbo wangu ulikuwa kwa ajili ya siku ya wapendanao, lakini nimewapigia honi wasanii ambao wanaona Zanzibar tuko nyuma kwamba tumeanza kuingia barabarani na huko tutashindana kwelikweli," amesema Sultan King.

# SAUTI ZA KUSHIBA KWENYE DANSI

**Na Adam Fungamwango**

KWENYE uimbaji kuna sauti za juu, za kati na zile za chini. Ukitaka uzifaidi sauti hizi vizuri basi upate waimbaji ambao wanaimba kwa staili ya kwaya.

Kwenye muziki wa dansi pia kuna utamu unaopatikana kutokana na waimbaji kuimba kwa kuitikia, kupokezana na kuimbisha mmoja mmoja.

Hii inafanya ladha ya aina yake kwenye muziki ambapo hupatikana ladha ya waimbaji wenye sauti za juu, za kati na hata zile za chini ambazo wataalamu wanaziita 'deep voice'.

Mara nyingi mashabiki wengi wa muziki huvutiwa zaidi na wanamuziki wenye sauti nyororo za juu. Lakini wapo wachache ambao huvutiwa na wanamuziki wenye sauti nzito na hasa wanapoimbisha au kuimba peke yao.

Leo tunawaletea wanamuziki wa dansi ambao wana sauti nzito zilizovutia mashabiki wengi nchini Tanzania.

**Hemed Maneti**

Alikuwa ni mwimbaji na kiongozi wa bendi ya Vijana Jazz. Ni mmoja ya wanamuziki wenye sauti nzito ambayo aliitumia vema na kuondokea kupendwa na kujizoela mashabiki wengi nchini.

Maneti ambaye alifariki Mei 31, 1990, jijini Dar es Salaam, alitunga na kuimba nyimbo mbalimbali ambazo zilimpatia umaarufu mkubwa.

Ukitaka uisikie vema sauti yake, tafuta zile ambazo aliimba peke yake baadhi ya vipande kama 'Vicky'. 'Masido', 'Tabu', 'Mundinde', 'Mary Maria', na nyingine nyingi ambazo zilimfanya kuwa staa Afrika Mashariki.

**Jerry Nashon 'Dudumizi'**

Huyu aliitwa 'Dudumizi' kutokana aina yake ya uimbaji ambapo sauti yake inafanana na ndege huyo, kutokana na staili yake ya kuitetemesha sauti yake nzito.

Ni mwimbaji na mtunzi aliyepitia bendi nyingi kama Magereza Jazz, Vijana Jazz, Bima Lee na nyinginezo.

Anatajwa kuwa ndiye mwimbaji mwenye sauti nzito zaidi kuliko wengine wote nchini Tanzania.

Nyimbo ambazo zimemtangaza sana na kujipatia mashabiki wengi ni 'Makulata', 'Baba Shani', 'Pendo', 'Pesa Zanisumbua' ambazo vipande virefu aliimba peke yake na kucheza vema na sauti yake nzito. Alifariki mwaka 1995 jijini Dar es Salaam.

**Muhidini Gurumo**

Ni mwimbaji nguli na mkongwe nchini Tanzania tangu miaka ya 60. Alifariki dunia 2014 na kuacha simanzi kwenye tasnia ya muziki nchini, akiimba miaka mingi zaidi kuliko mwanamuziki yoyote yule.

Huyu naye ni mmoja wa wanamuziki waliokuwa na sauti nzito zilizokuwa zikirindima kwenye redio nchini.

Ana nyimbo nyingi sana, lakini baadhi alizoziimba baadhi ya vipande peke yake ni 'Chatu Mkali', 'Rabana', 'Mv Mapezni namba moja', 'Isihaka' na nyingine nyingi.

**Adam Bakari**

Huyu alipewa jina la utani 'Sauti ya Zege' kutokana na kuwa na sauti nzito. Marehemu Adam Bakari alikuwa mwimbaji na mtunzi ambaye alipitia bendi nyingi na kuwa mmoja wa wanamuziki wanaoongoza kwa kuhama.

Ndiye mtunzi wa nyimbo maarufu nachi ambazo naye aliziimba kama 'Ogopa Tapeli', 'Azam Umeniumbua' za Vijana Jazz, lakini pia 'Nachelewa Stendi ya basi' wa Tomatoma.

**Mabrouk Mohamed**



Hakupata jina kubwa sana, lakini uakizisikiliza nyimbo za Mwenge Jazz Band utasikia sauti nzito ya Mabrouk Mohamed na kuwa ni mmoja wa wanamuziki wenye sauti za zege. Wakati wa mwishoni mwa uhai wake alipitia bendi ya TOT baada ya kustaafu jeshi la JWTZ na huko ndiko umauti ulipomfika.

FILAMU

# Vita ya Mapenzi: usilazimishe kupendwa

**Na Adam Fungamwango**

MAPENZI ni ridhaa baina ya mwanaume na mwanamke. Bila ridhaa hapo hakuna mapenzi, ila kuna utumwa. Mtumwa ni yule mtu ambaye anaishi sehemu asiyopenda, au mtu anayempenda kutoka moyoni mwake, ila kwa sababu amepelekwa kwa kulazimishwa au kuuzwa.

Kuna sababu gani ya kumlazimisha mtu kukupenda wakati hakutaki? Hata kama akikubali baadaye ni kwa sababu umemlazimisha. Penzi siku zote halisikiki, ila linaonekana. Wapenzi hawatumii nguvu nyingi ili wengine waone wanavyopendana. Ni wenyewe tu wanaona.

Leo tuiangalie filamu kali iitwayo 'Vita ya Mapenzi'. Ni vita kati ya vijana wawili, mmoja akipendwa na msichana na mwingine akilazimisha mapenzi.

Imechezwa na Said Lukamba, Vumilia Kasele, Sharif Adam, Rashid Mmambe, Halima Khalfan, Hajra Malila, Hadija Said na wengine wengi.

Kijana Lukamba anarejea kijiji kwao. Lakini akiwa na lengo moja tu kumuoa msichana wa kijiji cha pili aitwaye Olana.

Ni msichana ambaye mbali na kufahamiana wakitoka vijiji vinavyopakana, lakini pia waliwahi kukutana mjini kila mtu akiwa kwenye biashara zake.

Wazazi wa pande zote mbili wanapata taarifa kuwa vijana wao wanataka kuoana, kila mmoja anafurahi.

Barua ya posa inaletwa na mshenga ndani ila shilingi elfu sabini. Baba yake Olana anaila yote.

Baadaye inakuja kugundulika barua ile haikuwa ya Lukamba, bali kijana mwingine kijijini hapo aitwaye Makopa.

Huyo pia alikuwa anampenda Olana. Lakini binti alimpenda Lukamba. Makopa na Olana wanakutana njiani. Makopa anamuuliza, Olana anamwambia hawezi kubadilisha msimamo. Anakasirika na kutaka arejeshewe pesa zake za barua. Olana anamdhihaki kuwa kama angekuwa mwanaume kweli asingetaka arejeshewe. Makopa anaapa kulipiza kisasi.

Matayarisho ya harusi yanafanywa. Lengo ni kwamba waoane, halafu watimkie mjini wakaendelee kila mtu na biashara yake ambako walionana.

Makopa anacheza dili la rafiki yake kipenzi Lukamba kwa ahadi ya kumlipa pesa nyingi ili amsaliti. Dili linachezwa bi harusi anatekwa akiwa njiani akitoka saluni kupambwa.

Hali hii inaleta tafrani tupu na ugomvi mkubwa baina ya pande zote mbili za mwanaume na mwanamke. Bila kujua kila kitu kinafanywa kwa amri ya Makopa.

Baada ya kuona harusini hakueleweki ni ugomvi tu, huku mkewe mtarajiwa akiwa ametekwa, Lukamba anaamua kuingia kazini kumsaka mkewe. Hii ni sehemu ya kwanza ya filamu hiyo itakapotoka tuone nini kiliendelea.





# Trump amchefua Rihanna

INGAWA mashabiki na wapenzi wengi wa muziki wamefurahi kumuona mwimbaji mrembo, Rihanna akirejea jukwaani baada ya mapumziko ya miaka mitano, bado wamepigwa na butwaa baada ya kumuona akiwa na ujauzito.

Mmoja wa watu ambao hakufurahishwa ni rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, ambaye ameweka wazi kwamba hajafurahishwa naye.

Trump alitaja onyesho hilo kama faulo kubwa, wakati akishiriki kwenye mapitio ya kipindi cha mapumziko na wafuasi wake kwenye Truth Social, ambayo ni tovuti yake ya mtandao wa kijamii.



## Toyin akana kifo

MWIGIZAJI kutoka Nollywood, Toyin Abraham Ajewole ameshangaa baada ya kusambaa kwa taarifa kuwa amekufa.

Mwigizaji huyo alishirikisha picha iliyosambaa kwenye mtandao wa YouTube, ikitangaza kifo chake na kujibu kuwa ni mzima na anaweza kupiga kura.

"Kwa nini mtu yeyote aweke hii? Kwa nini? Kwa nini mtu yeyote awatakie wengine mabaya kwa sababu walifanya chaguo tofauti? Basi mimi bado nipo na nitapiga kura. Ameandika.

## Future ampa tano Tems

RAPA wa Marekani Future, amempongeza mwimbaji wa Nigeria Tems kwa mchango wake katika wimbo wake wa 'Wait For U.'

Wimbo huo ulishinda tuzo ya Utendaji Bora wa Melodic Rap katika tuzo za Grammy za 2023.

Kufuatia ushindi wake wa wimbo wa 'Wait for U,' mwimbaji huyo alikua msanii wa kwanza wa kike kutoka tasnia ya muziki ya Nigeria kushinda tuzo ya Grammy.





## Ini Edo wanamzushia tu

MTAYARISHAJI na mwigizaji kutoka Nollywood, Ini Edo, amekanusha kwamba yeye anaunga mkono tabia ya unyanyasaji dhidi ya wanawake.

Kufuatia maonyesho yake na hadithi katika mtandao wa Netflix, baadhi ya watu wamekuwa na maoni tofauti kuhusu filamu ya 'Shanty Town'.

Kulingana na Edo, anaamini kuwa usawa wa kijinsia ni jambo la kuzingatia na huwa mtetezi wa wanawake wanaonyimwa haki zao.

## Bruce hawezi tena kuigiza

FAMILIA ya Mwigizaji maarufu wa Marekani, Bruce Willis (67) imetoa taarifa kwamba nyota huyo hataweza tena kufanya kazi kutokana na kukabiliwa na tatizo la kiakili.

Taarifa hiyo iliyotolewa kupitia mitandao ya kijamii, ilisema staa huyo wa filamu za Hollywood, amepata ugonjwa wa akili unaojulikana kama Frontotemporal dementia ambao unamfanya kupoteza kumbukumbu na ufahamu wa mambo mengi.

Aidha, ilisema tatizo linalomkabili msanii huyo halina tiba ya moja kwa moja kwa mgonjwa wao, lakini wameamua kuweka wazi ili kuongeza ufahamu kwa Jamii kuhusu changamoto za magonjwa ya Afya ya akili

Nyota huyo alipata umaarufu kupitia filamu za Die Hard, The Sixth Sense na Armageddon.







## Kilio ukosefu CT Scan chamalizika

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HOSPITALI ya Rufani ya Mkoa wa Tanga ya Bombo, imemaliza tatizo lake la muda mrefu la kuwahamishia wagonjwa wake wanaotafuta huduma ya vipimo vya CT SCAN (Computerized Tomograph) katika Hospitali ya Taifa ya Muhimbili na Hospitali ya Rufani ya Kanda (KCMC).

Hatua hiyo ni baada ya serikali kutegua kitendawili hicho kwa kuipatia zaidi ya Sh. bilioni mbili.

Wagonjwa wa mkoa huo na wale wanaotokana na ajali za barabarani, walikuwa wakilazimika kupelekwa Kilimanjaro na Dar es Salaam kwa ajili ya kipimo hicho licha ya kuelezwa kwamba gharama zake zilikuwa juu na za kuumiza.

Mkuu wa Idara ya Mionzi na Picha wa Bombo, Dk. Goodluck Mbwilo, alisema jana kuwa uwekezaji huo mkubwa uliofanywa na serikali, umeandika historia mpya kwa mkoa huo, ambao haukuwahi kuwa na mashine kama hiyo.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuridhia kutupatia Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi wa jengo maalum na ununuzi wa mashine ya CT SCAN, kupitia fedha za Mradi wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

"Sasa hivi huduma za uchunguzi wa vipimo hivyo vinapatikana Bombo. Tumemaliza tatizo la kuwapa rufani wagonjwa kwenda mikoa mingine kufuata huduma hiyo. Tunawaarifu wakazi wa Tanga wachangamkie fursa ya kuwapo vipimo hivi ambavyo vimepunguza gharama kubwa ambazo awali walikuwa wakizitumia," alisema.

Mtaalamu wa mionzi wa hospitali hiyo, Athuman Rajabu, alisema CT Scan waliyoipata ina uwezo mkubwa wa kufanya uchunguzi kwa zaidi ya wagonjwa 100 kwa siku.

Alisema mara nyingi wagonjwa ambao hupata ajali za barabarani na magonjwa yasiyoambukiza kama saratani na kiharusi, walikuwa wanashindwa kujua yupi ana madhara zaidi au atapata nafuu.

# RC akataa bajeti bil. 41/- jiji Arusha

**Na Novatus Makunga,** RUSHA

MKUU wa Mkoa wa Arusha, John Mongella, ameukataa mpango na makisio ya bajeti ya makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri ya Jiji la Arusha ya mwaka ujao wa fedha 2023/2024, akisema haufanani na uhalisia wa vyanzo vyake.

Mpango wa bajeti aliouktaa ni uliokuwa upitishwe na Baraza la Madiwani wa zaidi ya Sh. bilioni 41, akieleza kwamba jiji hilo linapaswa kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 60.

Mongella alikuwa amealikwa jana katika mkutano maalumu wa baraza hilo lililoketi kujadili mipango na makadirio ya bajeti ya mwaka wa fedha wa 2023/2024.

Kigugumizi cha Mongella kuhusu bajeti hiyo, kilisababisha mkutano huo kuahirishwa huku akiwapa saa 72 wataalamu wa jiji kuandaa bajeti mpya.

Kabla ya kutoa amri hiyo, Mongella, alisoma barua ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Angellah Kairuki, kwenda kwa wakuu wa mikoa, inayoelekeza halmashauri za majiji, makusanyo ya mapato kwa mwaka ujao wa fedha yawe zaidi ya asilimia 35 ya bajeti ya mwaka uliopita.

Kwa mujibu wa rekodi za mkoa wa Arusha, mwaka wa fedha uliopita (2022/2023), Halmashauri ya Jiji lilikusanya Sh. bilioni 30.

Kutokana na maelekezo hayo, Mongella, alisema anaona kuna udhaifu mkubwa katika ukusanyaji wa mapato katika Halmashauri ya Jiji la Arusha, kutokana na kuwapo kwa mianya mingi ya ukwepaji wa kodi na ukusanyaji wa mapato, hivyo kuweka makadirio ya chini ya bajeti.

"Jiji la Arusha lina viwanda vingi vikubwa, ukusanyaji wa kodi ya huduma (service levy) ya asilimia 0.3 ya mapato ya wafanyabishara haifanyiki ipasavyo. Hata katika Kituo Kikuu cha Mabasi cha Arusha mambo ni hayo hayo.

"Kwa staili hii, naunda timu maalumu ya kuisaidia Halmashauri yenu kukusanya malimbikizo ya mapato, itakayoanza kazi Februari 20, mwaka huu, na kufanya kazi hadi Juni 31, mwaka huu.

"Timu itafanya kazi ya kukusanya mapato halali ambayo yanastahili kulipwa na kamwe haitamwonea mtu. Kitakachotakiwa ni kwa halmashauri kulipwa kile inachostahili," alisema.

Awali, Meya wa Jiji la Arusha, Maximillian Iranghe, alikiri kuwapo kwa udhaifu wa ukasanyaji wa mapato, akisisitiza udhaifu huo uko zaidi kwenye vyanzo vingi vya mapato, ambavyo havifikiwi kabisa, hivyo kuikosesha halmashauri hiyo mapato yake.

Alisema utafiti mbalimbali uliowahi kufanyika unaonyesha jiji lina uwezo wa kukusanya Sh. bilioni 62 na kwamba kama kutakuwa na mapato ya kutosha, linaweza kutekeleza miradi mingi ya maendeleo ambayo hutengewa asilimia 70 ya mapato yote ya ndani yanayokusanywa kila mwaka wa fedha.



Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba (katikati), akikata utepe kuzindua ugawaji wa vyandarua kwa wanafunzi wa shule za msingi za mkoani humo, katika viwanja vya Shule ya Msingi Mwenge jana. Wengine ni Meneja wa Bohari ya Dawa Mkoa huo, Siti Abdulrahman (wa pili kushoto), Meya wa Jiji la Tanga, Abdulrahman Shillow (kushoto), Ofisa Elimu wa mkoa, Mkisi Newaho (kulia) na Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashimu Mgandilwa. **PICHA: HAMIDA KAMCHALLA**

# Vifo vya watoto chini ya miaka mitano vyapungua

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI Msaidizi wa Wizara ya Afya, anayeshughulikia Masuala ya Watoto Dk. Filex Bundala, amesema vifo vya watoto chini ya miaka mitano nchini, vimepungua kutoka 147 kwa mwaka hadi kufikia vifo 43 kwa mwaka 2022.

Bundala alisema hayo jana jijini hapa wakati wa mkutano wa watalaam wa sekta ya afya kutoka nchi 25 ambazo zinatekeleza Mpango wa Udhibiti wa Magonjwa Chini ya Miaka Mitano kwa Watoto (IMCI).

Mradi huo unasimamiwa na Shirika la Afya Dunia (WHO) na wadau mbalimbali wakiwamo Shirika la Misaada la Maendeleo la Marekani (USAID) na Shirika la Kuhudumia Watoto la Umoja wa Mataifa (UNICEF).

"Kwa mujibu wa utafiti wa mwaka 2021 na 2022, kati ya watoto 1,000 walio chini ya miaka mitano, ni watoto 43 pekee ndiyo ambao walipoteza maisha ikilinganishwa na mwaka 1999. Katika mwaka huo, kati ya watoto 1,000 watoto 147 walipoteza maisha. Haya ni mafanikio makubwa ya kujivunia," alisema.

Dk. Bundala alisema mfanikio ya IMCI yanatokana na ushirikiano mzuri wa sekta mbalimbali katika kuhakikisha watoto chini ya miaka mitano wanapata huduma bora za afya kwenye vituo vya kutoa huduma, malezi na makuzi pamoja na upatikanaji wa huduma zingine muhimu.

"Mpango huu unatukumbusha mtoto anapofika kwenye kituo cha kutoa huduma za afya, afanyiwe uchunguzi wa kina kubaini ugonjwa unaomsumbua, apewe dawa stahiki, matumizi sahihi ya dawa, vituo kuwa na dawa kutosha lakini pia kuzingatia malezi na makuzi ya mtoto ikiwamo kupima uzito kulingana na umri, maneno ya kwanza anayoanza kuzungumza mtoto pamoja na upatikanaji wa huduma muhimu," alisema.

Alisema mpango huo wa kudhibiti vifo vya watoto chini ya miaka mitano nchini, ulianza kama majaribio mwaka 1996 lakini mwaka 1998, ulianza kuratibiwa nchi nzima lengo kuu likiwa ni kupunguza vifo vya watoto kwa magonjwa yanayotibika.

Dk. Bundala alitaja magonjwa ambayo yamekuwa yakisababisha vifo vya watoto kuwa ni magonjwa ya kawaida yanayotibika yakiwamo kuhara, malaria, vichomi (pneumonia), utapiamlo na maambukuzi ya virusi vya Ukimwi VVU.

"Kabla ya IMCI, asilimia 80 ya vifo vya watoto vilikuwa vinatokana na magonjwa ya kawaida ambayo yanatibika lakini baada ya kuwa na mpango wa kutumia chanjo na kutibu watoto kwa kutumia dawa moja au mbili ambazo zinaweza kutibu magonjwa ya aina tofauti kwa pamoja, tumefanikiwa kwa asilimia kubwa kudhibiti vifo vya watoto chini ya miaka mitano," alisema.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Enzi za ubunifu wa watoto wa kutengeneza, kurusha vishada

## -Ndipo msamiati 'halijojo' ulipotokea

Na Adam Fungamwango

KUNA mtu aliniandikia kuwa watoto wa zamani walikuwa wabunifu sana kwa sababu vitu vingine walikuwa wakitengeneza wao binafsi na kuvitumia, tofauti na sasa ambapo wengi hununuliwa na wazazi wao.

Akaanza na magari ya kuchezea, ambapo sasa yananunuliwa, tofauti na zamani mzazi wala hasumbuki kumnunulia mtoto gari la kuchezea, badala yake mtoto mwenyewe anaenda kuchimba udongo, kukusanya maboksi makopo na kutengeneza magari ya kuchezea.

Na walifanya hivyo kwa ustadi wa hali ya juu, kiasi kwamba pamoja na kwamba ni la kuchezea watoto, lakini ukilitazama taswira yake ni kama gari, lori au basi.

Matairi yake yalitengenezwa kwa kandambili ambazo zinakatwa duara, hapo gari la kuchezea linakuwa limekamilika. Wale watoto wa zamani ambao kwa sasa ni watu wazima nadhani watakuwa tayari wameshaelewa walikuwa wanafanya nini hadi wakawa wanaunda magari ya kuchezea ambayo yalikuwa yanashindana uzuri kwa muonekano.

Aliyeniandikia meseji pia akasema kwa sasa watoto wa sasa wana mchezo wa kupuliza kitu kinaitwa 'bubble', ambapo wananunua au kununuliwa 'super market', wakati wao zamani walibuni kufanya michezo hiyo kwa kutumia vibomba vya majani ya mpapai na maji ya sabuni.

Ni kweli kabisa, watoto zamani walikuwa wanachukua maji safi, halafu wanachanganya na sabuni kwa hiyo yanakuwa na mapovu.

Unachukua kibomba cha mti wa papai, unakata saizi unayoitaka. Unachofanya ni kuweka mdomoni kibomba hicho, halafu ncha nyingine unaingiza kwenye maji ya sabuni na kuvuta kidogo. Baada ya hapo unatoa, halafu unapuliza.

Kinachotoka ni viputo ambavyo vinatoka kwenye kibomba na kuruka juu. Wakati mwingine vinatoka viwili, au vitatu kwa mpigo. Ni michezo tu ya watoto kujifurahisha enzi hizo. Hii ipo kwa sasa, lakini hivyo vitu wanavigharamia badala ya kufanya ubunifu.

Nikirudi tena nyuma kulikuwa na mchezo maarufu sana kwa watoto enzi hizo. Huu ni kutengeneza na kurusha tiara.

Watoto wa miaka ya 1990 kurudi nyuma watakuwa wanajua nini nakiandika hapa. Na neno



tiara halikutumika sana, ila watoto wa enzi hizo walitumia neno kishada.

Watoto walikuwa bize kweli na vishada. Ulikuwa ni moja ya michezo maarufu sana na ukazaa msamiati wa halijojo ambao umekuwa ukitumia sehemu mbalimbali, hata kwenye siasa.

Kishada ni kitu mfano wa ndege ambacho kinapaa angani kwa kutumia upepo.

Kila mmoja alikuwa na utengenezaji wake. Lakini wengi walitengeneza kwa kutumia magazeti na miti myembamba, huku nyuma unaweka kama mkia hivi,

Pembeni mwa eneo la tumbo kwenye zile pembe, kuna vikaratasi ambavyo vinaning'inia baada ya kutengenezwa kwa ustadi mkubwa.

Baada ya hapo watoto wanakifunga kishada kwa kamba ya uzi mrefu mno, na kama haupatikani kuna kamba za viroba nazo pia zilitumika.

Mara nyingi watoto walikuwa wanakwenda sehemu zenye uwazi ili kupata upepo unaotakiwa, halafu anakiachia na kufungua kamba.

Kishanda kinaanza kupaa kikielekea ambapo upepo unaelekea. Hapo ndipo utamu wenyewe wa mchezo wa kishada unapokuwa.

Yule mwenye kishada chake kwenda juu na mbali zaidi ndiyo anaonekana anajua sana na mshindi. Mara nyingi unakuwa si ufundi sana, bali kamba yake inakuwa ndefu zaidi kuliko wengine.

Kuna wakati mpaka kishada chenyewe kukiona juu inakuwa shida. Mrushaji akisharidhika na kamba ameimaliza, anakwenda kufunga kwenye mti au kukandamizia jiwe na anabaki akiangalia kinavyopepea juu angani, basi ni furaha moyoni, wimbo mdomoni.

Starehe nyingine ilikuwa kuteka kishada cha watoto wengine. Mnatengeneza kamba ndefu mnaifunga jiwe mwishoni, halafu unarusha lile jiwe juu ya kamba ya kishada mnachotaka kukiteka, kazi imekwisha.

Wakati huo kulikuwa na msemo kuwa "kishada changu kimekwenda halijojo." Ulikuwa ukitumika kwa watoto kuelezea kuwa kamba imekatika kwenye kishada chake, kwa hiyo kinapepea tu juu. Iko hivi.

Kishada kwenda halijojo, maana yake unapotaka kurusha ni lazima uwe na uzi ambao ni mgumu na hautakatika kirahisi, halafu unapokipaisha kitapaa kulingana na urefu wa kamba ile, pia upepo uwemkali kidogo, ule uzi ukifika mwisho, mpaishaji huridhika na hata kufunga uzi kwenye mti ulio karibu akaendelea na shughuli zake zingine bila kujali kinahitaji uangalizi na umakini wa kutambua ya kwamba ile kamba inaweza kukatika wakati wowote.

Sasa kamba ikikatika kwa bahati mbaya kishada ndiyo kinakwenda halijojo, yaani bila muelekeo.

Kifuatacho, mwenye kishada anaanza kukikimbiza mtaa hadi mtaa bila kujali wala kufahamu ni umbali gani kitadondokea.

Ndiyo maana tunaweza kuusikia msamiati huu kwa watu wa kada mbalimbali, mfano hata wanasiasa wakati mwingine wakisema " wale chama chao kinakwenda halijojo" Maana yake ndiyo hiyo.

Tuma meseji 0716 350534

## Marekani yagoma kuomba radhi

**WASHINGTON,** MAREKANI

RAIS wa Marekani Joe Biden amesema haombi radhi kwa kudungua puto linalodaiwa kuwa la kijasusi la China lilokuwa likipaa kwenye pwani ya Marekani.

Alisema puto hilo lilitumika kwa uchunguzi, lakini vitu vingine vitatu vilivyodunguliwa juu ya nchi za Amerika Kaskazini haviwezi kuwa vya kijasusi.

Alisema nchi yake sasa inaboresha ugunduzi wake wa vitu sawa na hivyo vya angani.

Biden pia alisema atazungumza na Rais wa China Xi Jinping, hivi karibuni kuhusu tukio hilo la mwezi huu.

"Natumai tutafikia mwisho wa hili, lakini siombi radhi kwa kudungua puto hilo," Biden alisema akiwa Ikulu ya 'White House' juzi.

China imekanusha kuwa puto hilo lilitumika kwa uchunguzi, badala yake ilisema lilipoteza mkondo wake wakati wa kukusanya data ya hali ya hewa.

Lakini Rais Biden alisisitiza maoni ya maofisa wa Marekani kwamba puto hilo, ambalo lilivuka nchi katika mwinuko wa takriban futi 40,000 kabla ya kudunguliwa kutoka angani na ndege ya kivita ya Marekani juu ya ya bahari ya Atlantiki.

Alisema Marekani inaendelea kuzungumza na China kuhusu suala hilo, lakini hawatazamii kuibuka kwa vita baridi vipya.

**BBC**

# Afrika Kusini, Russia, China zaanza mazoezi makali ya kivita

**CAPE TOWN, AFRIKA KUSINI**

AFRIKA Kusini, Russia na China zimeanza jana mazoezi ya kivita ya pamoja, hatua ambayo imeanza kuwapa hofu nchi za Magharibi.

Wakitumia meli kubwa ya kivita inayoitwa "Admiral Gorshkov" ambayo imetia nanga kwenye bandari ya Cape Town, wanajeshi wa nchi hizo tatu wameanza mazoezi hayo yatakayomalizika Februari 27.

Mazoezi hayo ya pamoja ni ya pili kufanyika yakihusisha vikosi vya jeshi la maji la Russia, Afrika Kusini na China.

Mazoezi ya kwanza yalifanyika mwaka 2019. Uhusiano wa kihistoria kati ya Russia na chama tawala cha Afrika Kusini, ANC unaweza kuelezea msimamo wa Rais Cyril Ramaphosa.

Luteka hiyo inayoitwa "Mazoezi ya Pili ya Mosi", inayomaanisha moshi kwa lugha ya Kitswana, inaenda sambamba na kumbukumbu ya mwaka mmoja tangu Russia ilipoivamia Ukraine Februari 24.

Hatua ya Afrika Kusini kujiunga katika mazoezi hayo imewatia wasiwasi washirika wa Magharibi ambao wanaipa misaada nchi hiyo. Mkuu wa sera za kigeni wa Umoja wa Ulaya, Josep Borell alisema katika mkutano wake wa pamoja na Waziri wa Mambo ya Nje wa Afrika Kusini, Naledi Pandor kwamba mpango wa luteka hiyo ya jeshi la majini halikuwa jambo zuri.

Naibu Mkurugenzi wa Mradi wa Taasisi ya Kimataifa ya kushughulikia Migororo, ICG barani Afrika, Pauline Bax, alisema ingawa serikali ya Afrika Kusini haijazungumzia chochote kuhusu luteka hiyo, ukweli ni kwamba kufanyika kwa mazoezi hayo wakati wa kipindi cha mwaka mmoja tangu kuanza kwa vita vya Ukraine, ni jambo la kutatanisha.

Bax aliambia DW kwamba wanadiplomasia wengi wa Magharibi wanaona mazoezi hayo ya kijeshi kama yanayopingana na madai ya Afrika Kusini ya kutoegemea upande wowote.

Waziri Pandor, mara ya kwanza alilaani uvamizi wa Urusi nchini Ukraine, lakini Rais Ramaphosa alimlazimisha kubatilisha kauli yake na kumpokea waziri mwenzake wa Russia, Sergei Lavrov kwa heshima zote mwishoni mwa mwezi Januari.

Uhusiano kati ya Russia na Afrika Kusini ni wa muda mrefu baada ya kukiunga mkono chama cha ANC wakati wa mapambano ya kupinga ubaguzi wa rangi nchini humo.

Joe-Ansie van Wyk, profesa wa Siasa ya Kimataifa katika Chuo Kikuu cha Afrika Kusini, UNISA mjini Pretoria, alisema nchi hiyo ina lengo la kuimarisha uhusiano wake na Russia na China ambao ni wanachama wa kudumu wa Baraza la Usalama la Umoja wa Mataifa, ambako bara la Afrika kwa muda mrefu limetoa wito wa kuwa na sauti zaidi.

Van Wyk ameiambia DW kwamba Afrika Kusini ni sehemu ya kundi la nchi zinazoinukia kiuchumi za BRICS, inayozijumuisha Russia, India, China na Brazil.

Bax alisema vita vya Ulaya havitishii usalama wa Afrika na nchi za Afrika hazitaki kulazimishwa kuchagua upande wowote, ingawa vita vya Ukraine vilikuwa na madhara kadhaa barani Afrika, ikiwemo kupanda kwa bei ya mafuta na vyakula. Hivyo hali inaweza kuwa mbaya zaidi.

Nchi nyingi za Afrika zinahisi kwamba zinaweza kuwa na washirika tofauti, hazitaki kuchaguliwa upande wowote ule.

**(DW)**



Watu wakikusanya baadhi ya mali zao katika vifusi vya nyumba iliyoanguka baada ya tetemeko la ardhi katika mji wa Atareb, nchini Syria. **PICHA: AP**

# Mgomo wasababisha maelfu kushindwa kusafiri Ujerumani

**BERLIN, Ujerumani**

MGOMO wa wafanyakazi wa viwanja vinane vya ndege nchini Ujerumani, umesitisha usafiri na kulazimisha mashirika ya ndege kufuta safari zao.

Wafanyakazi katika viwanja hivyo wameanza mgomo huo jana wakishinikiza kuongezewa mishahara na kuboreshewa mazingira ya kazi.

Mgomo huo ulioanza jana uliitishwa na chama cha wafanyakazi cha Verdi umeilazimisha kampuni kubwa ya ndege nchini Ujerumani, Lufthansa kufuta safari zipatazo 1300 katika viwanja vya Frankfurt na Munich ambavyo ndivyo vyenye shughuli nyingi.

Viwanja vingine vilivyoathirika vipo katika miji ya Bremen, Dortmund, Hamburg, Hanover, Leipzig na Stuttgart. Maelfu ya wasafiri wanakabiliwa na uwezekano wa safari zao kucheleweshwa au kufutwa kabisa.

Shirika la viwanja vya ndege Ujerumani, ADV, limeulaani mgomo huo likisema haukubaliki na kuongeza kwamba utawaathiri wasafiri 295,000 na jumla ya safari za ndege 2,300.

Chama cha wafanyakazi cha Verdi kinataka wafanyakazi waongezewe malipo wakati huu ambao mfumuko wa bei umeshusha thamani ya mishahara yao na kuzidisha ugumu wa maisha.

**DW.**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**JAMARI NEMES MSIGALA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba: **S2135/0020** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **LUHUNDWA SECONDARYSCHOOL** mwaka 2017. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **DOD/DOD/RB/401280/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**MAJUTO KATWANGA MBUYA** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne chenye Index **NO. S1933/0043/2018** kilichotolewa na baraza la Mitihani kupitia NYASATO SECONDARY SCHOOL mwaka 2018. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **GEI/MBO/RB/446381/2021**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO**

**WILAYA YA MOROGORO, MKOA WA MOROGORO**

**Usimamizi wa Mirathi Na......12/2023**
**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU: JUMA ALLY KAFERA WA KIHONDA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA USIMAMIZI WA MIRATHI YALIYOLETWA NA KAPEZIWA ABDALLAH FUNDIKIRA**

**TANGAZO**
**(kanuni ya 5(2)ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu,wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tahehe 21 Mwezi 02 Mwaka 2023 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

**Zingatia;**

- Wosia wa marehemu huyo upo mahakaman na waweza kukaguliwa
- Marehemu hakuacha wosia wowote.

Imetolewa leo tarehe 17 mwezi 02 mwaka 2023

HAKIMU MKAZI
MAHAKAMA YA MWANZO KIHONDA
MOROGORO
.....................................
HAKIMU

## TANGAZO TANGAZO

**Kiwanja kinauzwa.** Kipo **Kiwalani Jet Lumo.** Km 12 kutoka Posta Mpya. Ukubwa ni **337.5 Sqm. Bei 70m.** Kinafaa kwa makazi na biashara. Barabara nzuri ya lami yenye taa, hakuna foleni kwenda posta na maji ni ya DAWASA. Wasiliana na **0753064048.**

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**IN THE DISTRICT REGISTRY**
**AT MUSOMA**

**LAND APPEAL NO. 35 OF 2022**

(arising from the decision of the District Land and Housing Tribunal for Mara in Land Appeal No. 159/2021, Originating from land case No. 18od 2021 at Nyakatende Ward Tribunal)

**BUDIGO FIDELI..........................................APPELANT**

**VERSUS**

**JOHN MALIMA............................................RESPONDENT**

TO: JOHN MALIMA
C/O VEO NYAKATENDE VILLAGE,
P.O.BOX 1061,
MUSOMA

**SUMMONS FOR PUBLICATION**

**WHEREAS** the Appellant have filed an appeal against you, you hereby summoned to appear in this court in person or by pleader duly instructed and able to answer all material questions relating to the appeal or who shall be accompanied by some person able to answer all such questions on the 9th day of March 2023 at 10:00am o'clock in the forenoon before Hon. F.H.MTULYA, judge to answer the case.
Take notice that in default of your appearance on the day before mentioned, the Appeal will bw heard and determined in your absence
Given under my hand and the seal of the court this 23rd day of Nvember 2022

DEPUTY REGISTRAR
MUSOMA

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**Ndugu John Kamata** Mahega wa Bariadi Simiyu anatangaza kupotelewa kwa kadi ya gari lake aina ya Toyota Succed yenye namba za usajili **T594 DJM** Taarifa imetolewa kituo cha polisi Maswa kwa namba,**SIM/MAS/RB/245788/2021** yeyote atakayeiona au kuiokota awasiline naye kwa namba **0784776456** au aipeleke kituo chochote cha karibu naye ,

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA YA BUKOBA MKOA WA KAGERA**

**MAOMBI MADOGO NA. 103/2020**

**MARTIN MUGANYIZI EDWARD (Msimamizi wa mirathi ya marehemu) EDWARD NSHEKIBWEKI ................MWOMBAJI**

**DHIDI YA**

**HELENA SILIVERY**
**SOSPETER DANIEL BYARUGABA .............WAJIBU MAOMBI**

**KWA: HELENA SILIVERY NA SOSPETER DANIEL BYARUGABA (POPOTE PALE MLIPO)**

Mnaarifiwa kuwa maombi Na. 103/2020 yamepangwa kutajwa terehe 21/02/2023 mbele ya Mwenyekiti wa Baraza, P.J. Makwandi saa 2:00 asubuhi. Hivyo mnaamuriwa kuhudhuria nyinyi wenyewe/ mwakilishi wenu mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Msipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yenu na hukumu kutolewa.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na Muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08/02/2023.

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**AHMED SAID BAMAGA** anatangaza kupotea kwa kadi za gari zenye usajili namba **T733 BEN, T163 AGJ, T 674 AGS.** Kwa yeyote atakaeziona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/60744/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**AHMED SAID BAMAGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki yenye usajili namba: **MC946BBM.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/60744/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BRIGHTON MHANDU MGUNDA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA ISIS** yenye usajili namba **T 248 DPM ,** CHASSIS NAMBA: **ZNM100020340** na ENGINE NAMBA: **1ZZ2289235 .** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/URA/RB/6626/2023**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya wilaya ya GEITA**

**Kituo cha NYANKUMBU Mkoa GEITA**

**Shauri la Madai Na 8/2023**

**Jina la Mdai:GEORGE MHANGILWA**

**Jina la Mdaiwa EMMANUEL SHIGANGA**

**KUITWA SHAURINI MDAIWA**
**(Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo)**

**Kwa EMMANUEL SHIGANGA WA BUKOLI**

Kwa kuwa Mdai ameleta madai yake kwamba (Eleza hapa habari za Madai) **NG'OMBE WAWILI WENYE THAMANI YA TSH. 1,300,000/-**
Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 20 Mwezi 02 Mwaka 2023 Saa 08:30 asubuhi/Mchana kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

**ANGALIZO:** Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini,Mahakama inaweza kusikiliza shauri hili bila ya wewe kuwepo

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 10 Mwezi 02 Mwaka 2023

RESIDENT MAGISTRATE
GEITA.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MERY TARISISI**

Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 511BLD TOYOTA HILUX .** Chasses Namba **RZN 1470020622 ,** Engine Namba **IRZ3274929**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taafifa :
**KIL/MOS/RB/64024/2023**

**IN THE DISTRICT COURT OF KOROGWE**
**AT KOROGWE**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO...03.... OF 2023**

**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE ELIYA MATHAYO JOHO**

**AND**

**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATIX**
**BY MATHAYO JOHO MBAGO**

**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules GN 369 OF 1963)**

All PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 13 Day of March, 2023

Dated at KOROGWE this 13 day of February, 2023

DISTRICT COURT
KOROGWE

**OFISI ZA MATANGAZO**

**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**

**PO.BOX 31042,**

**DAR ES SALAAM.**

**MOB: +255 - 745 700 710.**

**E-mail: advertise@guardian.co.tz,**

**website: www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0745 700 710.***

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako la Nipashe kila siku Tupigie

Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji na kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yanayopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

# MTAKE MSITAKE-19

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

"Kikao kilifanyika nikamatwe, nilazishwe kuondoka, au niuawe. Niliwasiliana na Makao Makuu na wakaniambia nifanye chochote kile lakini nisiondoke hadi nikamilishe misheni, lakini nizuie nisitekwe, kufukuzwa wala kuuawa. Pamoja na hayo walinionya nisizuie vitu hivyo kwa kutumia nguvu, labda kupambana nao, bali akili na hila zaidi kwa sababu hawakutaka yoyote yule ahisi labda mimi si mtu wa kawaida."

Wakati akiongea maneno hayo watu walikuwa kimya, wengine wakionyesha mshangao kwa kile walichokuwa wakikisikia.

"Mpango namba moja nilioona unafaa ni kujifanya kipofu. Siku zote ambazo mlidhani kwamba mimi ni kipofu si kweli. Ulikuwa ni mpango mkakati ili Usonzo asiniteke wala kufanya chochote kwangu ili niendelee kuifanya kazi ya upelelezi kwa amani na uhuru zaidi. Ukweli uliokuwepo hapa mimi si kipofu."

Alisema na kuvua mawani yake. Aliweka fimbo yake pembeni na kushuka chini kwa kasi akipiga hatua moja kwa moja kwenye ngazi na kupandisha tena.


Hili lilisababisha umati wote ulipuke kwa nderemo na vifijo, huku baadhi wakionekana kama wanaangalia filamu, wasiamini kile kilichotokea.

Aliporudi kila kitu alikiweka pembeni. Sasa aliongea kama mtu mzima na si mlemavu wa macho tena. Mawani aliweka pembeni.

"Jamani mpango huu niliufanya kwa kushirikiana na Mary kwa ajili ya kumzuga Usonzo na kweli alizugika na ilinisaidia kwa pande zote mbili. Nilimwambia Mary najifanya kipofu na yeye ndiye ionekane amenimwagia tindikali ili wote wawili, mimi na yeye tuishi kwa amani kwenye kijiji kwa sababu angeonekana kufurahishwa na tukio hili. Na kweli ndivyo ilivyokuwa."

Umati wa watu waliokuwa na mshangao uliochanganyika na furaha uliendelea kumtazama na kumsikiliza Adel.

"Mpango mkakati ulifanyika hivi. Nilimfuata Mary na kumwambia kwa sababu anapendwa na Usonzo, na anahisi sisi ni wapenzi, basi tutengeneze uongo kuwa amenimwagia tindikali kwa sababu ya




**"Taarifa zimeshanifikia, nilikuwa nataka kupata uthibitisho ni nani. Ngoja nikulize swali. Kwa nini umemwagia tindikali wakati ni mpenzi wako?"**

kumsumbua na kumfuatafuata huku akijua ana mapenzi wake. Vyovyote ambavyo watu wangetafsiri kama ambavyo walitafsiri. Tukaongea na Mganga Mkuu wa Mkoa athibitishe tukio hili ili watu wasiwe na wasiwasi kuwa jambo hili ni la kupangwa. Mganga Mkuu ndiyo mtu kwa kwanza kuambiwa dhamira ya tukio hilo ni kukiokoa kijiji chote, kwa sababu alikuwa akihofu kukiuka maadili, lakini nilimwambia hii ni kwa maslahi ya Taifa, ndipo alipokubali kuingia kwenye mpango mkakati huu. Tukio lilifanyika kweli, lakini nilichomwagiwa ni maji ya kawaida tu ya bomba, na nikajifanya jioni nimepofuka, na haraka Mary aliita ndugu zake na wangu nikakimbizwa hospitali na daktari kwa sababu ameshaambiwa kitakachofanyika, akathibitisha na kusema tayari nimekuwa kipofu.

Habari zilipovuja, kila mtu akaongea lake. Wengine walisema nimemwagiwa na Enock kwa sababu amegundua nimemchukulia mchumba wake. Wengine wakasema amemwagiwa na Mary mwenyewe kwa kuhofia kujulikana kwa Enock kuwa tuna mahusiano ya kimapenzi. Na wapo waliosema Enock aliweka mtego, na Mary akaona ili awe salama, basi akaamua kufanya hivyo ili kuua soo. Mary akajitokeza na kukiri hadharani na kusema kuwa atanitunza. Ulikuwa ni mpango namba mbili kuwa niendelee kuwa naye, ili tuweze kufanya kazi kirahisi.

Umati uliendelea kuwa kimya, sasa ukianza kujua kumbe ile kumwagiwa Adel tindikali ulikuwa ni mchongo tu na si tukio la kweli.

"Kusema kweli mpango huu ulitusaidia sana, Usonzo akaacha kunifutilia ili anidhuru, na hii ilinipa uhuru mkubwa wa kuendelea kupeleleza mambo. Akaamua kumpongeza kabisa Mary kwa tukio alilofanya. Lakini akamshauri eti anifukuze, lakini akamwambia anafanya hivyo ili nisiende kushtaki.

Tukapanga kwa makusudi Mary aende kwa Usonzo amdanganye na uongo aliokwenda kuuzungumza ni huo. Kwa bahati nzuri Mary alipokwenda kwenye ofisi za Usonzo alikuwa akirekodi kila kitu bila mwenyewe kujua. Hebu sikilizeni maongezi haya ambayo waliyaongea alipofika, Usonzo akidhani ni kweli aliyokuwa akiongea Mary, kumbe ulikuwa ni mtego tulioupanga.

Alitoa kitu mfano ya redio ndogo, akabonyeza kitufe, ikasogezwa kwenye maiki, hivyo sauti zilizokuwa zikitoka kwenye kitu hicho ya mwanaume na mwanamke zilisikika kwenye spika kubwa.

*****************************

"Usonzo nimekuja, naomba unisaidie kwa hili.".

"Umekuja leo kijana eee, mtoto matata sana wewe, unayekataa hata matajiri. Haya kuna nini leo?"

"Naomba unisaidie kuniokoa kwenye hili janga, vinginevyo naweza kufungwa."

"Wewe sema, usizunguke mrembo." Usonzo akaunguruma.

"Mimi ndiye niliyemwagia Adel Adam tindikali, yule kijana mgeni na madaktari wamethibitisha kuwa amekuwa kipofu. Hatoona tena milele. Sasa taarifa zimeshafika kwa Mwenyekiti wa Kijiji mzee Chale, nimesikia kesho nitaitwa. Naogopa atakwenda kupeleka taarifa hizi kituo cha Polisi mkoani."

"Taarifa zimeshanifikia, nilikuwa nataka kupata uthibitisho ni nani. Ngoja nikulize swali. Kwa nini umemwagia tindikali wakati ni mpenzi wako?"

"Hapana, siyo mpenzi wangu. Ni kweli alikuwa ananitaka, lakini hakuwa mpenzi wangu."

"Siyo kama umeamua kufanya hivyo ili kufuta ushahidi?"

"Hapana mzee Usonzo, yule kijana aliniokoa kwenye ajali ya bodaboda, ndiyo nikafahamiana naye. Kuna siku nilikutana naye nikiwa na mchumba wangu Enock, nikamtambulisha. Wakawa marafiki, kuna wakati wakawa wanatembeleana na yeye akawa anaweza kuja hata kwetu. Akatumia njia hiyo kunitongoza. Nilimkatalia, akawa anazidi kufanya hivyo, nikaona hali ikizidi kubwa mbaya Enock akijua itakuwa matatizo, siku moja akaja nyumbani, anakawa ananishikashika, kwa hasira, nikaenda kuchukua tindikali ya baba alikuwa kuna sehemu kaificha, nikamwagia."

"Enhee, sasa wewe ulitaka mimi nifanye nini?"

"Nataka umzuie mzee Chale asilipeleke suala hili Polisi.

ITAENDELEA JUMAMOSI

# NBC YAKABIDHI BASI JIPYA KWA KMC, MAKALLA ATAKA LITUNZWE

**Na Mwandishi Wetu**

BENKI ya Taifa ya Biashara (NBC) ambayo ni mdhamini Mkuu wa Ligi Kuu Tanzania Bara, jana ilikabidhi basi jipya kwa timu ya KMC FC ya Kinondoni jijini Dar es Salaam inayoshiriki ligi hiyo, huku Mkuu wa Mkoa huo, Amos Makalla akipongeza hatua hiyo.

Hafla ya makabidhiano ya basi hilo lenye thamani ya Sh milioni 450 lililotolewa kama mkopo kutoka benki ya NBC ilifanyika jijini Dar es Salaam na kuhudhuriwa na wadau mbalimbali wakiongozwa na Makalla, viongozi wa Shirikisho la Mpira Miguu Tanzania (TFF), pamoja na Mkurugenzi Mtendaji wa Benki hiyo, Theobald Sabi. Akizungumza kwenye hafla hiyo, Makalla, aliipongeza benki hiyo kwa jitihada zake za kuiboresha ligi hiyo, huku akitoa wito kwa klabu mbalimbali nchini kuitumia vema benki ya NBC kutatua changamoto zinazowakabili kama vile usafiri na Bima kwa wachezaji na benchi la ufundi. "Kila mtu sasa ni shuhuda kwa namna ambavyo ligi yetu imekuwa bora tangu kuanza kwa udhamini wa NBC. Inafurahisha zaidi kuona udhamini huo hauishii tu kwenye ligi pekee bali pia benki inaguswa na changamoto za timu moja moja, hongereni sana NBC. Naomba sana timu nyingine pia ziige mfano huu wa KMC bila kujali ukubwa wao," alisema Makala huku akitoa wito kwa uongozi wa timu hiyo kuhakikisha wanarejesha mkopo huo kwa wakati.

Awali akizungumza kwenye hafla hiyo, Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Sabi alisema hatua hiyo imekuja baada ya kikao baina ya benki hiyo na klabu zote zinazoshiriki ligi hiyo ikiwemo KMC na kuunda fursa wezeshi za kusaidia timu kujikwamua na changamoto mbalimbali ikiwemo ya usafiri wa uhakika.

"Ligi hii inahusisha suala zima la usafiri kwa klabu husika na wakati mwingine timu zinasafiri kwa umbali mrefu sana na hivyo kusababisha uchovu kwa wachezaji. Upatikanaji wa mabasi mazuri ya kisasa utasaidia kupunguza uchovu kwa wacheza ili waweze kuleta ushindani unaohitajika wakiwa viwanjani. Leo hii tumeanza na KMC ila bado klabu nyingine zitafuata," alisema Sabi.

Aidha Sabi alisema ukosefu wa vyombo vya usafiri maalum kwa ajili ya timu zinazoshiriki ligi hiyo imekua ni moja ya chanzo cha vikwazo vingi katika gharama za uendeshaji na utendaji wa timu husika.

Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule pamoja na kuishukuru benki hiyo kwa mkopo huo aliihakikishia kuwa wamejipanga kuhakikisha kwamba unarejeshwa kwa wakati huku pia akiahidi kulitunza vyema basi hilo.

Akizungumzia ujio wa basi hilo, Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni, Songoro Mnyonge alisema limepatikana wakati muafaka na kwamba litamaliza kabisa changamoto ya usafiri iliyokuwa ikiikabili klabu hiyo pale inapohitaji kucheza mechi za mikoa ya mbali.




Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla (wa pili kushoto) akipokea mfano wa ufunguo wa gari kutoka kwa Mkurugenzi Mtendaji wa NBC, Theobald Sabi (kushoto) ikiwa ni ishara ya kukabidhiwa basi jipya lililotolewa na benki hiyo kwa njia ya mkopo kwenda kwa timu ya KMC FC inayoshiriki ligi Kuu ya Tanzania. Wengine ni pamoja na Mkuu wa Wilaya ya Kinondoni, Saad Mtambule (wa tatu kushoto), Mstahiki Meya wa Manispaa ya Kinondoni Songoro Mnyonge (wa tatu kulia), Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni, Hanifa Hamza (wa pili kulia) na Mkurugenzi wa wateja wadogo wa NBC, Elibariki Masuke (Kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# *BMT yahimiza uwazi kwa vyama vya michezo*

**Na Saada Akida**

KATIBU Mtendaji wa Baraza la Michezo la Taifa, Neema Msitha amevitaka vyama vya michezo kufanya mambo yao kwa uwazi na uwajibikaji kwa ajili ya kuwavutia wadhamini na wadau kuwasaidia.

Msitha ametoa kauli hiyo baada ya Taasisi ya Maajabu 18 kutoa seti mbili za jezi jumla ya 56 pamoja na fedha za usafiri kwa chama cha mchezo wa Kabadi.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu huyo alisema kitendo cha Chama cha Kabadi kuweka wazi changamoto zao imechangia kupatikana kwa wadhamini.

Alisema baada Chama hicho kuingia udhamini na Chuo cha St. Joseph ambacho kilitoa ofisi na kuahidi usafiri wa timu ya Taifa.

"Kitendo hicho kimewavutia uongozi wa Taasisi ya maajabu 18 na walinipigia simu na kutaka kuwa sehemu ya udhamini wa mchezo huo kupitia ligi yao inayotarajia kuanza hivi karibuni," alisema Neema.

Alisema kujitokeza kwa mdhamini huyo ni kutokana na uwazi wa mambo yanayofanywa na Chama husika na kuvitaka vyama vingine kufanya mambo yao kwa uwazi na kuiga mfano wa Kabadi.

Kwa upande wa Msimamizi wa Taasisi ya maajabu 18, Mussa Athuman alisema kwa kuanza wametoa jezi seti mbili na kuwasaidia katika mambo ya kiuchumi katika safari yao ya kuelekea michuano ya kombe la Dunia.

Mwenyekiti wa Mchezo wa Kabadi Taifa, Abdallah Nyoni alisema ni jambo la furaha kupata udhamini huo.

"Tunaenda katika Ligi, hivyo kuna uhitaji mkubwa wa vifaa na jezi hizi zitatusaidia kwa sababu zinaenda kwa klabu ya Buffalo, huku Chama kikiendelea na mchakato wa kutafuta wadhamini wengi kupata vifaa kwa klabu zingine ," alisema Nyoni.

## Judo yajipanga michuano ya Afrika

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Judo Tanzania (JATA), kinatarajia kushiriki michuano ya Afrika itakayofanyika nchini Tunisia mwishoni mwa mwezi ujao.

Akizungumza na gazeti hili jana, Katibu Mkuu wa Jata, Innocent Mallya alisema ili kupata wachezaji wa kuwakilisha nchi katika michuano hiyo, watachagua wale watakaofanya vizuri kwenye michuano ya Afrika Mashariki, inayotarajiwa kufanyika nchini mapema mwezi ujao.

"Tunategemea kushiriki mashindano ya Afrika ni muhimu kwetu kutengeneza viwango vya wachezaji, vile vile tutaangalia wale ambao watafanya vizuri kwenye mashindano yajayo na wale wenye uzoefu mkubwa ambao tumekuwa nao," alisema Mallya.

Alisema maandalizi kuelekea kwenye mashindano hayo ya Afrika Mashariki yanakwenda vizuri na hadi sasa nchi tano zimethibitisha kushiriki.

Alizitaja nchi hizo kuwa ni Tanzania, Zanzibar, Burundi pamoja na Rwanda huku wakiendelea kusubiri nchi nyingine hadi kufika Machi mosi mwaka huu ziwe zimetoa taarifa ya ushiriki wao.

Judo ni miongoni mwa michezo yenye bahati ya kushiriki mashindano ya kimataifa ingawa bado haijafanya vizuri kama ilivyo upande wa Afrika Mashariki ambapo wamekuwa wakishika nafasi ya kwanza, ya pili na tatu mara kadhaa.

## Oppa: Kila mechi ya Simba Queens ni fainali

**Na Saada Akida**

NAHODHA na kinara wa mabao wa Simba Queens, Oppa Clement amesema akili na nguvu za wachezaji wote wanachukulia kila mechi kwao ni fainali na kuhitaji pointi tatu katika michezo ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania Bara.

Oppa aliibuka kuwa mchezaji bora wa Januari akiwa na mabao 9 akiongoza kwa ufungaji na timu yake ikiwa kileleni mwa msimamo kwa pointi 22.

Akizungumza na gazeti hili jana, Oppa alisema ligi hiyo msimu huu imekuwa ya ushindani mkubwa na kila mchezaji anatambua umuhimu wa kila mechi watakayocheza.

Alisema makocha wanaendelea kufanyia kazi mapungufu yao na kuongeza ubora uliokuwapo kwa kikosi ili kufanikiwa malengo yao ya kutetea taji la ubingwa.

"Ligi msimu huu ngumu kila mechi kwetu tunaichukulia fainali, lazima kupambana kutafuta matokeo ya ushindi kwa ajili ya kufikia malengo yetu ya kutetea ubingwa," alisema straika huyo.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### MESSI SAFI PSG

BABA wa nahodha wa Argentina, Lionel Messi alifanya mazungumzo na PSG siku ya Alhamisi huku akitarajia kuafikiana kuhusu mkataba mpya wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 35. (***Mail***)

### NEYMAR NA EPL

KLABU kadhaa za Ligi Kuu England, EPL, vimearifiwa kuhusu uwezekano wa kupatikana kwa mshambuliaji wa Paris St-Germain wa Brazil, Neymar mwenye umri wa miaka 31. (***90min***)

### MOUNT AFUATILIWA

LIVERPOOL, Manchester City na Manchester United zinafuatilia hali ya mkataba wa kiungo wa kati wa England, Mason Mount mwenye umri wa miaka 24 katika klabu ya Chelsea. (***ESPN***)

### QATAR OFA YA MWISHO

WAWEKEZA wa Qatar wanatayarisha ofa ya mwisho yenye thamani ya takriban pauni bilioni 5 kwa ajili ya kuinunua Manchester United. (***Bloomberg***)

### SABITZER PAUNI MIL 18

KLABU ya Bayern Munich imeiambia Manchester United kwamba, itahitaji kulipa pauni milioni 18 kumnunua kiungo wa kati wa Austria, Marcel Sabitzer mwenye umri wa miaka 28 kwa mkataba wa kudumu. (***Bild, via Mail)***

### DALOT ATAKIWA MADRID

KLABU ya Real Madrid inatazamia kumnunua beki wa Manchester United na Ureno, Diogo Dalot mwenye umri wa miaka 23, ambaye bado hajaongeza mkataba wake Old Trafford. (***AS***)

### ROQUE AWINDWA

ARSENAL imetuma wasaka vipaji wao kumfuatilia mshambuliaji wa kimataifa wa vijana wa Athletico Paranaense na timu ya taifa ya Brazil, Vitor Roque. Barcelona pia inamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 17 ambaye ada yake huwenda ikawa pauni milioni 50. (C***aughtOffside***)

### KVARATSKHELIA AVUTIA

KLABU za Newcastle, Real Madrid, Manchester City na PSG zinavutiwa na winga wa Napoli na Georgia, Khvicha Kvaratskhelia, lakini klabu hiyo ya Serie A inataka zaidi ya pauni milioni 50 kumwachia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. (***90min***)

### ANCELOTTI HAJALI KWA ASENSIO

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti amesema hajali iwapo kiungo wa Hispania, Marco Asensio mwenye umri wa miaka 27, atasaini mkataba mpya katika klabu hiyo au ataondoka. (***Mirror***)

### MOFFI ANYATIWA

KLABU za Southampton na West Ham zinawasiliana na wawakilishi wa mshambuliaji wa Nice, Terem Moffi, mwenye umri wa miaka 23. (***Football Insider***)

### REDKNAPP KUREJEA

KOCHA wa zamani wa Tottenham Hotspur, Harry Redknapp atakuwa tayari kurejea kwenye uongozi iwapo Leeds United itamtaka arejee uwanjani. (***Mirror***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# NEYMAR SASA KUTUA EPL

**LONDON,** England

●●● Klabu za Man City, Man United na Chelsea zapigana vikumbo kuwania saini yake...

NIA ya Neymar kutaka kuhamia Ligi Kuu ya England, EPL, inazidi kushika kasi, huku Manchester City, Manchester United na Liverpool zikiwa miongoni mwa timu zilizonesha nia ya kumhitaji.

**Nyota huyo mwenye umri wa miaka 31 aliripotiwa kuwa alihusishwa katika mazungumzo ya hivi majuzi kati ya mmiliki wa Chelsea, Todd Boehly na rais wa Paris Saint-Germain Nasser Al-Khelaifi.**

Neymar hadi sasa amefunga mabao 10 kwenye Ligi Kuu ya Ufaransa, huku akifikisha mabao 12 katika mechi 19 za mashindano yote.

Sasa katika msimu wake wa sita nchini Ufaransa tangu awasili kwa ada iliyovunja rekodi ya dunia ya euro milioni 222, mfungaji huyo bora wa muda wote wa Brazil anakodolea macho changamoto mpya.

Kwa mujibu wa 90min, "wawakilishi wa Neymar wanafanya mazungumzo na Chelsea, Liverpool, City, United, na Newcastle United" - kuziarifu klabu hizo kuhusu nia ya mchezaji huyo kuhamia Ligi Kuu ya England.

Ripoti hiyo inadai Paris Saint-Germain hawana tatizo kuachana na Neymar na watakuwa tayari kukamilisha zoezi hilo.

Mmiliki wa Chelsea, Boehly anaaminika kuwa na "shauku" kuhusu uwezekano wa kumsajili Neymar na atakuwa tayari kufikia mahitaji yatakayotakiwa kwenye mkataba.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,077,4
MSHINDI WA SUPA JACKPOT YA MECHI - 13




KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa vodacom m-pesa halopesa airtel money
SEND
SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 18+ HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# TEN HAG, RASHFORD WALIA NA MWAMUZI SARE YA BARCELONA

**MANCHESTER,** England

ERIK ten Hag alikasirishwa na uamuzi wa mwamuzi wa kutoipa Manchester United nafasi ya kupiga mpira wa adhabu ndogo baada ya Marcus Rashford kuchezewa vibaya kwenye sare ya 2-2 dhidi ya Barcelona kwenye Uwanja wa Camp Nou, katika mchezo wao wa kwanza wa raundi ya mtoano ya Ligi ya Europa, juzi.

Rashford alikuwa mwiba kwa Barca kwa muda wote na alionekana kuchezewa faulo na Jules Kounde nje kidogo ya eneo la hatari huku United wakiwa mbele kwa mabao 2-1, lakini mwamuzi Maurizio Mariani aliruhusu mchezo uendelee.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alisawazisha bao la kwanza la Marcos Alonso mapema kipindi cha pili kabla ya kulazimisha bao la kujifunga la Kounde kuipatia United uongozi, ingawa Raphinha alisawazisha zikiwa zimesalia dakika 14.

Licha ya matokeo chanya kwa ujumla, Ten Hag aliona haja ya kuangazia tukio lililohusisha Kounde kumchezea faulo Rashford.

Ten Hag aliambia BT Sport: "Nadhani mwamuzi alikuwa na ushawishi mkubwa kwenye mchezo huu.

"Unaweza kujadili kama ilikuwa ndani au nje ya boksi, na kwa njia yoyote ilikuwa ni kadi nyekundu kwa sababu (Rashford) alikuwa ana kwa ana na kipa.

"Kwa hiyo ni ushawishi mkubwa, sio tu kwa mchezo huu, katika mzunguko huu. Haiwezi kuwa, waamuzi hawawezi kufanya makosa kama hayo."

Rashford mwenyewe vile vile alishangazwa na uamuzi wa Mariani.

"Ni wakati mkubwa katika mchezo," alisema. "Sijaitazama tena lakini kwa sasa sielewi ni kwanini hatukupewa nafasi ya kupiga mpira wa adhabu ndogo.

"Alinigusa wakati mguu wangu uko mbele ya mpira, (Kounde) akaupiga mguu wangu na ni nikashindwa kusonga mbele. Sio penalti lakini ni faulo kwa asilimia 100 kwangu."

Hata hivyo, Ten Hag alikubali ubora wa jumla wa pambano hilo la kusisimua na alifurahishwa na wingi wa nafasi ambazo United ilitengeneza.

"Nadhani tuliamuru mchezo," Ten Hag aliendelea. "Mbali na labda dakika 15 za kipindi cha kwanza tulikuwa na shida, lakini kwa wengine tuliamuru mchezo."

# *Llorente atundika daruga akiwa na miaka 37*

**MADRID,** Hispania


MSHAMBULIAJI wa zamani wa Juventus, Athletic Bilbao na Hispania, Fernando Llorente amestaafu kucheza soka akiwa na umri wa miaka 37.

Llorente - ambaye amekuwa bila klabu tangu mwisho wa msimu uliopita - alitangaza kupitia Movistar Plus kwamba, umefika mwisho wake wa kucheza baada ya miaka 18 kwenye mchezo wa soka.

Llorente alianza maisha yake ya soka akiwa na Athletic, ambapo alicheza kwa misimu tisa kwenye kikosi cha kwanza, akifunga mabao 84 katika michezo 262 ya Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga.

Kisha akahamia kwa wababe wa Serie A, Juventus, ambapo alifunga 16 katika mechi 34 za ligi katika msimu wake wa kwanza, ingawa hakuweza kurudia kiwango hicho kabla ya kuondoka kwa uhamisho wa bure na kurejea Hispania kwenye Klabu ya Sevilla mwaka 2015.

Baada ya msimu mmoja kwenye



Uwanja wa Ramon Sanchez Pizjuan, ambapo alifunga mabao manne pekee katika mechi 23 za LaLiga huku akishinda taji la Ligi ya Europa, Llorente alihamia Ligi Kuu England kwenye klabu ya Swansea.

Alifunga mabao 15 ya ligi katika mechi 33 akiwa na Swansea kabla ya kutimkia Tottenham Hotspur baada ya mwaka mzuri huko Wales.

Llorente hakuwa na wakati mzuri wa kupata mechi za kucheza pale Spurs, lakini alichukua jukumu muhimu katika mbio zao za fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019, akifunga bao lililoifanya Spurs kutinga nusu fainali dhidi ya Manchester City.

Llorente hakuweza kurejea katika ubora wake wa awali alipokuwa Napoli au Udinese, kabla ya kucheza ule uliokuwa msimu wake wa mwisho kurejea Hispania akiwa na Eibar.

Alishinda mataji matatu ya Serie A, mataji mawili ya Coppa Italia na Ligi ya Europa wakati wa maisha yake ya kilabu.

Llorente pia alikuwa sehemu ya kikosi cha Hispania kilichoshinda Kombe la Dunia la 2010 na Euro 2012, akiichezea nchi yake mechi 24 kwa jumla, akifunga mabao saba..

# HABARI MICHEZO

33,324/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 18/02/23 | 18:00 | Blackpool vs Stoke City | 2.70 | 3.25 | 2.55 |
| 02. 18/02/23 | 18:00 | Huddersfield Town vs Birmingham City | 2.65 | 3.25 | 2.55 |
| 03. 18/02/23 | 18:00 | Everton FC vs Leeds United | 2.36 | 3.30 | 2.95 |
| 04. 18/02/23 | 18:00 | Hull City vs Preston North End | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 05. 18/02/23 | 18:30 | Portimonense SC vs Maritimo Madeira | 2.29 | 3.15 | 3.15 |
| 06. 18/02/23 | 20:00 | FC Winterthur vs FC Sion | 2.45 | 3.10 | 2.44 |
| 07. 18/02/23 | 20:30 | CD Leganes vs UD Las Palmas | 2.70 | 2.90 | 2.80 |
| 08. 18/02/23 | 20:30 | Newcastle United vs Liverpool FC | 2.27 | 3.45 | 2.95 |
| 09. 18/02/23 | 20:30 | RCD Mallorca vs Villarreal CF | 3.15 | 2.95 | 2.42 |
| 10. 18/02/23 | 20:45 | FC Groningen vs FC Emmen | 2.28 | 3.20 | 3.10 |
| 11. 19/02/23 | 14:15 | SC Cambuur vs SC Heerenveen | 3.05 | 3.25 | 2.31 |
| 12. 19/02/23 | 15:00 | Motherwell FC vs Heart of Midlothian FC | 2.80 | 3.25 | 2.47 |
| 13. 19/02/23 | 16:00 | SD Huesca vs Granada CF | 3.30 | 2.95 | 2.34 |
| 14. 19/02/23 | 16:00 | Elche CF vs Espanyol Barcelona | 2.75 | 3.05 | 2.60 |
| 15. 19/02/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Montpellier HSC | 2.50 | 3.20 | 2.75 |
| 16. 19/02/23 | 18:15 | Rayo Vallecano vs Sevilla FC | 2.43 | 3.00 | 3.05 |
| 17. 19/02/23 | 18:30 | Santa Clara Azores vs FC Famalicao | 2.80 | 3.15 | 2.55 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE
"2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 18/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 1291 | Perth Glory vs Central Coast Mariners | 2.97 | 3.28 | 2.31 |
| 15:30 | 3678 | Aston Villa vs Arsenal | 4.01 | 3.40 | 1.86 |
| 15:30 | 5992 | Millwall vs Sheffield Utd | 2.63 | 3.28 | 2.53 |
| 16:00 | 4112 | Coastal Union vs Mbeya City | 2.23 | 2.86 | 3.30 |
| 16:00 | 4980 | Real Sociedad vs Celta Vigo | 1.78 | 3.35 | 4.79 |
| 16:00 | 5666 | Parma vs Ascoli | 1.81 | 3.33 | 4.43 |
| 17:00 | 5403 | Sampdoria vs Bologna | 3.08 | 3.03 | 2.35 |
| 17:30 | 2424 | Monchengladbach vs Bayern Munchen | 6.35 | 5.36 | 1.36 |
| 17:30 | 3204 | VfL Bochum vs SC Freiburg | 2.97 | 3.42 | 2.22 |
| 17:30 | 3616 | VfL Wolfsburg vs RB Leipzig | 3.13 | 3.43 | 2.13 |
| 17:30 | 3905 | Stuttgart vs FC Koln | 2.36 | 3.32 | 2.82 |
| 18:00 | 1643 | Ipswich vs Forest Green | 1.26 | 5.52 | 9.46 |
| 18:00 | 1734 | Nottingham vs Manchester City | 8.35 | 4.90 | 1.32 |
| 18:00 | 1774 | Brentford vs Crystal Palace | 1.84 | 3.43 | 4.08 |
| 18:00 | 1860 | Brighton vs Fulham | 1.64 | 3.87 | 4.76 |
| 18:00 | 1888 | Luton Town vs Burnley | 3.18 | 3.23 | 2.19 |
| 18:00 | 1893 | Huddersfield vs Birmingham | 2.57 | 3.11 | 2.71 |
| 18:00 | 2000 | Middlesbrough vs QPR | 1.61 | 3.77 | 5.16 |
| 18:00 | 2529 | Blackburn vs Swansea | 2.62 | 3.31 | 2.52 |
| 18:00 | 2791 | Sheffield Wed vs MK Dons | 1.44 | 4.26 | 6.73 |
| 18:00 | 3561 | Hibernian vs Kilmarnock | 1.73 | 3.74 | 4.39 |
| 18:00 | 3743 | Wigan vs Norwich City | 3.32 | 3.37 | 2.07 |
| 18:00 | 3769 | Derby vs Charlton | 1.58 | 3.97 | 5.16 |
| 18:00 | 3850 | Hull City vs Preston | 2.14 | 3.22 | 3.32 |
| 18:00 | 3984 | Chelsea vs Southampton | 1.36 | 4.55 | 8.12 |
| 18:00 | 4079 | Celtic vs Aberdeen | 1.14 | 7.55 | 14.90 |
| 18:00 | 5054 | Wolverhampton vs Bournemouth | 1.63 | 3.66 | 5.15 |
| 18:00 | 5280 | Royal Antwerp vs Eupen | 1.35 | 4.89 | 7.79 |
| 18:00 | 5342 | Sunderland vs Bristol City | 2.02 | 3.37 | 3.47 |
| 18:00 | 5397 | Livingston vs Rangers | 7.96 | 4.88 | 1.34 |
| 18:00 | 5431 | Rotherham vs Coventry | 3.17 | 3.32 | 2.16 |
| 18:00 | 5517 | Blackpool vs Stoke City | 2.82 | 3.26 | 2.39 |
| 18:00 | 5933 | Everton vs Leeds | 2.39 | 3.21 | 2.86 |
| 18:15 | 1663 | Lugo vs Eibar | 3.85 | 3.01 | 2.05 |
| 18:15 | 3234 | Betis vs Valladolid | 1.60 | 3.85 | 5.40 |
| 18:30 | 5699 | Portimonense vs Maritimo | 2.26 | 3.29 | 3.04 |
| 19:00 | 1854 | Kagera Sugar vs Namungo | 2.29 | 2.73 | 3.36 |
| 19:00 | 2767 | Nice vs Reims | 2.11 | 3.27 | 3.37 |
| 20:00 | 3135 | Monza vs AC Milan | 3.46 | 3.26 | 2.07 |
| 20:30 | 2320 | Mallorca vs Villarreal | 3.19 | 2.89 | 2.43 |
| 20:30 | 3943 | Eintracht Frankfurt vs Werder Bremen | 1.58 | 4.17 | 4.86 |
| 20:30 | 4632 | Newcastle vs Liverpool | 2.45 | 3.42 | 2.63 |
| 20:30 | 4832 | Leganes vs Las Palmas UD | 2.63 | 2.88 | 2.83 |
| 21:00 | 4117 | Dijon vs Metz | 3.22 | 3.12 | 2.23 |
| 22:45 | 1388 | Union Saint Gilloise vs Standard Liege | 1.54 | 4.09 | 5.58 |
| 22:45 | 4101 | Inter vs Udinese | 1.49 | 4.25 | 5.73 |
| 23:00 | 1316 | Strasbourg vs Angers | 1.87 | 3.38 | 4.08 |
| 23:00 | 3730 | Osasuna vs Real Madrid | 4.39 | 3.54 | 1.79 |
| 23:00 | 5981 | Feyenoord vs AZ Alkmaar | 1.70 | 3.82 | 4.37 |
| 23:30 | 2329 | Porto vs Rio Ave | 1.17 | 6.59 | 14.97 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

## UWANJA WA MKAPA KUBORESHWA KWA AJILI YA AFRICA SUPER LEAGUE

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeahidi kufanya marekebisho makubwa yanayohitajika katika uwanja wa Benjamin Mkapa ili kukidhi viwango vya kimataifa vinavyohitajika katika michuano ya Africa Super League ambayo Klabu ya Simba ndio mwakilishi wa ukanda wa Afrika Mashariki.

Hayo yamesemwa jana jijini Dar es Salaam na Katibu Mkuu wa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo, Saidi Yakubu wakati alipokutana na uongozi wa Shirikisho la Soka Afrika (CAF) ambao unaongozwa na Mkuu wa Kitengo cha ufundi, Mohammad Sidat alieambatana na wataalaam kutoka Italia waliokodiwa na Shirikisho hilo.

Yakubu alisema kuwa maeneo yote yaliyoainishwa yatafanyiwa kazi kabla ya ziara nyingine ya ukaguzi itakayofanywa na CAF.

Pia aliwaeleza viongozi hao kuwa serikali inakusudia kujenga viwanja vingine vya michezo na watategemea sana miongozo ya kitaalamu toka Shirikisho la soka la Kimataifa, Fifa na CAF.

Kwa upande wao, Ujumbe huo wa CAF waliarifu kuhusu hatua za haraka zinazotakiwa kufanywa ili uwanja uendelee kutumika kimataifa na kupongeza maendeleo ya soka nchini.

Uongozi wa klabu ya Simba uliandaa hafla hiyo ya chakula cha jioni iliyohudhuriwa pia na Naibu Spika, Mussa Azzan Zungu kwa nia ya kufanya tathmini baada ya ukaguzi kufanyika.



Wageni kutoka nje ya nchi na (kushoto) viongozi wa Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni, Dar es Salaam, wakicheza ngoma wakati wa mapokezi ya wageni hao juzi, walipotembelea kituo kujifunza jinsi ambavyo kinaendesha vita dhidi ya ukatili wa kijinsia. **PICHA: SABATO KASIKA**

## Tutawasha moto leo

INATOKA UK 24

etupa motisha kubwa kwa kutuahidi fedha na hivyo sisi wachezaji hatupaswi kumuangusha.

"Naomba nimuhakikishie Rais wetu kwamba wachezaji wote tumeahidi kupambanana tuko tayari kupata ushindi mbele ya Raja Casablanca," aliongeza Bocco.

Alisema watakuwa makini katika kuzuia na kushambulia kwa sababu ya kuhakikisha wanaendeleza kauli yao ya uwanja wa Mkapa hatoki mtu hasa mechi za kimataifa.

Kwa upande wake Mkuu wa Casablanca, Modher Keboir alisema wataingia kwa tahadhari kubwa kwa sababu Simba sio timu ya kubeza na ina uwezo mkubwa.

"Simba ni timu kubwa na tumejiandaa vizuri, tutaingai kwa tahadhari kubwa na kuhakikisha tunapata matokeo mazuri," alisema Keboir.

## Yanga kupambana jasho na damu kuiua Mazembe

INATOKA UK 24

ilopeleka na badala yake wakakodisha mabasi madogo mawili aina ya Coaster, Privadinho alisema wao wametekeleza wajibu wao, na yaliyotokea hayawahusu.

"Hawa ni watu wazima, basi limeletwa hawakutaka kupanda wamepanda kwenye mabasi madogo, wamechagua walichokiona wao ni sahihi. Sababu ya kufanya hivyo mimi sijui labda muwaulize nyinyi kwa nini hawakupanda," alisema.

Kwenye tukio hilo, basi liliiloletwa na uongozi wa Yanga kwa ajili ya wageni halikutumiwa na wachezaji, badala yake walipanda mashabiki wa TP Mazembe.

Mchezaji wa zamani wa Yanga, Mukoko Tunombe alisema anajisikia vizuri kurejea tena nchini Tanzania kucheza dhidi ya timu yake ya zamani, akidai mechi itakuwa ngumu, lakini yeye anawafahamu vilivyo Yanga.

"Kuhusu Mukoko kuifahamu Yanga na kuonekana siyo tatizo kwa sababu hata sisi tuna wachezaji kutoka Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ambao wanaifahamu vema TP Mazembe na pia tunamfahamu Mukoko," Privadinho alijibu mapigo.

Kesho Yanga itacheza mechi ya pili ya Kombe la Shirikisho Afrika kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, kuazia majira ya 1:00 usiku.

# Michezo

Nipashe Jumamosi Februari 18, 2023




Neymar sasa kutua EPL

UKURASA 21



Wachezaji wa Simba wakifanya mazoezi katika Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam jana kujiandaa na mchezo wake wa Klabu Bingwa Afrika dhidi ya Raja Casablanca leo. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Tutawasha moto leo

## ●●● Ni wakati Simba ikiwashukia Raja Casablanca, wachezaji waahidi pointi tatu, mamilioni ya Rais Samia yawa motisha kubwa...

**Na Saada Akida**

POINTI tatu ni lazima. Hii ni kauli ya Wanasimba wote wakiongozwa na benchi la ufundi chini ya Kocha, Robert Oliveira kuelekea mchezo wa leo dhidi ya Raja Casablanca ukiwa ni wa pili kwao katika hatua ya makundi ya Ligi ya mabingwa Afrika.

**Simba watakuwa wenyeji katika mchezo huo utakaopigwa uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam kuanzia majira ya saa 1:00 usiku.**

Kikosi hicho cha Simba kinashuka dimbani kikiwa na kumbukumbu ya kupotea mchezo wa kwanza kwa bao 1-0 kutoka kwa Horoya AC kwenye uwanja wa Gnrl Lansana Conte Conakry nchini Guinea wiki iliyopita.

Katika mchezo huo, Simba ilikosa huduma ya kiungo mshambuliaji, Saido Ntibazonkiza kwa sababu ya kutoka huku Mosses Phiri akicheza dakika chache na kutoka majeruhi.

Katika mechi ya leo Kocha Robertinho ana uwezekano mkubwa wa kuwanyamazisha nyota hao wawili katika kuongoza safu ya ushambuliaji ili kuhakikisha wanapata ushindi dhidi ya Raja Casablanca.

Licha ya kuwepo kwa wachezaji hao, Wekundu wa Msimbazi hao watakosa huduma ya kiungo wao mkabaji, Sadio Kanoute akitumikia adhabu ya kadi mbili za njano.

Simba ipo kundi C katika nafasi ya tatu ikiwa haina pointi, huku Casablanca inaongoza kundi ikiwa na pointi tatu na mabao matano ambayo waliyapata dhidi ya Vipers ya Uganda katika mchezo wa kwanza wa kundi hilo.

Akiuzungumzia mchezo huo, Robertinho alisema kila mchezo wa michuano hiyo ni mkubwa na una uzito mkubwa na ushindani, hivyo leo wanahitaji pointi tatu dhidi ya Casablanca.

Alisema Simba ni timu kubwa kama ilivyo Casablanca na ameiandaa timu yake kwa ajili ya kushinda mchezo huo ili wapate nafasi ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

"Kumkosa mchezaji wa kutumainiwa kama Kanoute ni pigo, lakini kwa sababu tuna kikosi kipana tumeweza kumpata mbadala wake," alisema kocha huyo.

Aliongeza: "Tunacheza nyumbani, lazima tutafute ushindi, matumaini yangu ni kwamba tutapata matokeo mazuri, nina waheshimu wapinzani wetu, katika hii michuano hakuna mchezo rahisi."

Kwa upande wa Nahodha wa Simba, John Bocco alisema wameshamaliza maandalizi, na anaamini mchezo utakuwa mgumu kwa sababu wapinzani ni wazuri, lakini wao wanahitaji pointi tatu na watapambana kuzipigania.

Alisema ili kujitengenezea mazingira mazuri na kusonga mbele lazima washinde mechi ya leo dhidi ya Casablanca na kuendelea na rekodi yao ya kutumia vizuri uwanja wa nyumbani.

"Tumeshafanya mazoezi mazuri na mbinu tulizopewa na benchi la ufundi, tunahitaji pointi tatu muhimu na tunaimani kushinda mchezo wetu dhidi ya Casablanca," alisema Bocco.

"Pia tuna ari kubwa kutokana na kauli ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan ambapo am-

INAENDELEA UK 23

# Yanga kupambana jasho na damu kuiua Mazembe

**Shufaa Lyimo na Adam Fungamwango**

NAHODHA wa Yanga, Dickson Job amesema watapambana kwa jasho na damu kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo wao wa kesho Jumapili dhidi ya TP Mazembe kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Yanga itashuka dimbani kesho kwenye uwanja wa Benjamin Mkapa kwenye mchezo wake wa pili wa hatua ya makundi ya michuano hiyo, baada ya ule wa kwanza kufungwa bao 2-0 na US Monastir ya nchini Tunisia, kwenye kundi D.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam kuelekea mchezo huo, Job alisema wamejipanga kupata ushindi kwenye uwanja wa nyumbani.

"Huu utakuwa ni mchezo wa kumwaga jasho na damu ili kuhakikisha tunapata ushindi, wachezaji wote tuna ari kubwa sana kuelekea mchezo huu," alisema Job.

Aliongeza: "Tumejianda vya kutosha na lazima ushindi upatikane kwa sababu tutakuwa kwenye uwanja wetu wa nyumbani ambao tumeuzoe."

Job aliongeza kuwa kutokana na mazoezi wanayoendelea kuyafanya anaamini hakuna litakaloshindikana.

Alisema licha ya kuwa walipata matokeo mabaya kwenye mchezo wao wa kwanza na timu ya US Monastir, bado hawajakata tamaa na badala yake wamepata molari kubwa zaidi.

Wakati huo huo, klabu yaTP Mazembe ya Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo ilitua nchini juzi na kukataa basi waliloandaliwa na wenyeji wao Yanga.

Msimamizi Mkuu wa Digitali na Maudhui wa Yanga, Priva Abiud maarufu kama Privadinho ambaye alikuwepo uwanja huo kama mmoja wa maafisa wa klabu hiyo kwa ajili ya mapokezi alitoa wito kwa wanachama na mashabiki wa timu yake kujazana kwa wingi uwanjani ili iwe kama chachu zaidi ya kupata ushindi kwenye mchezo huo.

"Nimekuja hapa nimeona mashabiki wa TP Mazembe wanashangilia. Mashabiki wa Yanga wanapaswa kujua kuwa wenzao hawako nyuma, umeona wametua tu hapa uwanja wa ndege wanashangilia, kama hapa Uwanja wa Ndege ni hivi huko uwanjani wa soka itakuwaje? Kwa maana hiyo nawasihi mashabiki wetu waje uwanjani kwa wingi Jumapili kuishangilia timu yao," alisema Privadinho.

Akizungumzia tukio la wachezaji wa TP Mazembe kukataa basi wal-

INAENDELEA UK 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >